
SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Biteko** aanika ukweli jiwe la rubi la Dubai

UKURASA 3




Jumapili Aprili 24, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe
MWANGA WA JAMII
JUMAPILI
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • No. 0580925
twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Waeleza namna ya kumuenzi Nyerere

UKURASA 2



"Ninashukuru nimezaliwa na wazazi wema mmoja ametangulia mbele ya haki na mwingine bado yupo.

**Makongoro Nyerere**



"Mwalimu Nyerere alipenda dini lakini alikwepa kuingiza siasa ndani yake, alikuwa mwadilifu, mwenye nidhamu ya hali ya juu, alikuwa na uongozi jumuishi na alipenda kusikiliza.

**Warioba**



"Mwalimu Nyerere katika kipindi chote cha uhai wake aliwaunganisha Watanzania akiamini umoja, upendo na mshikamano pamoja na kudumisha amani ni msingi muhimu na bora.

**Dk. Mwinyi**



"Wazee na wanazuoni watumie midahalo, mihadhara na kuandika makala, majarida na vitabu kwa lengo la kuhakikisha urithi wa maisha ya Hayati Mwalimu Nyerere unatambulika, kuhifadhiwa na kusherehekewa.

**Majaliwa**



"Isingekuwa misingi imara aliyoiweka Hayati Mwalimu Nyerere ambayo ni amani, utulivu na kujitegemea basi tusingekuwapo hapo.

**Makala**

## Wanandoa wafariki wakiwa usingizini chanzo kikidaiwa ni jiko la mkaa

UKURASA 3



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka.

## Kigogo wa PAC ashtuka madudu ripoti ya CAG

• **Aomba** kamati nyeti za Bunge zipewe muda mrefu kuichambua... *Endelea ukurasa 2*

MICHEZO SIMBA, ORLANDO MUDA UMEFIKA UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6




Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Woodrow Wilson International Center, Balozi Mark Green, katika mdahalo uliofanyika katika ofisi za taasisi hiyo, jijini Washington, Marekani juzi. **PICHA: IKULU**

# Waeleza namna ya kumuenzi Nyerere

**Na Romana Mallya**

VIONGOZI waandamizi wa serikali wamesema Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, aliwaunganisha Watanzania huku akichukia rushwa, ufisadi, uonevu, dhuluma na ubaguzi.

Wamesema katika kurithisha vizazi vijavyo falsafa zake, wazee na wanazuoni waendelee kuandika makala, majarida na vitabu kwa lengo la kuhakikisha urithi wa maisha yake unatambulika, kuhifadhiwa na kusherehekewa.

Wakizungumza jana katika maadhimisho ya miaka 100 ya kuzaliwa kwa Hayati Mwalimu Nyerere yaliyoandaliwa na Mama Maria Nyerere nyumbani kwake, Msasani, Dar es Salaam, viongozi hao walieleza sababu ya kukumbukwa kwa kiongozi huyo.

Sherehe hizo zilibebwa na ujumbe usemao, '1922-2022 Ulikuwa Zawadi Kubwa Kwetu Familia, Taifa, Afrika na Ulimwengu.'

Miongoni mwa waliohudhuria ni pamoja na viongozi wa serikali, Chama Cha Mapinduzi (CCM), mabalozi, wapigania uhuru, wasomi, maofisa wa jeshi waliobeba jeneza la Hayati Mwalimu Nyerere na baadhi ya wafanyakazi wake wa wakati huo.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ambaye alikuwa mgeni rasmi alisema njia bora ya kumkumbuka Hayati Mwalimu Nyerere ni kutekeleza kwa vitendo urithi aliowaachia.

"Tutamkumbuka namna alivyojitoa muhanga kupigania ukombozi na ujenzi wa taifa hili kwa kushirikiana kwa pamoja na marehemu Amani Abeid Karume. Walisimamisha nguzo imara za Muungano wetu ambao wiki ijayo (Aprili 26) tutasherehekea miaka 58 tangu kuasisiwa kwake," alisema.

Dk. Mwinyi, alisema Hayati Mwalimu Nyerere katika kipindi chote cha uhai wake aliwaunganisha Watanzania akiamini umoja, upendo na mshikamano pamoja na kudumisha amani ni msingi muhimu na bora.

"Alichukia uonevu, dhuluma na ubaguzi wa kila aina, alichagua lugha ya Taifa letu kuwa ni Kiswahili akiamini kwamba ni lugha ya kutuunganisha na kutangaza utamaduni wetu. Alitumia uhai wake kusisitiza umuhimu wa kuwa na siasa na mipango ya kujenga uchumi unaojitegemea na matumizi bora ya rasilimali," alisema.

Pia alisema Mwalimu Nyerere aliamini umuhimu wa kuimarisha misingi ya utawala bora kwa kupiga vita rushwa, uzembe ufisadi wizi na ubadhirifu wa mali za umma na atakumbukwa kwa juhudi za kuongoza wapigania uhuru barani Afrika na kuimarisha umoja wa waafrika.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alitoa wito kwa wazee na wanazuoni kutumia njia za midahalo, mihadhara na wakati mwingine kuandika makala, majarida na vitabu kwa lengo la kuhakikisha urithi wa maisha ya Hayati Mwalimu Nyerere unatambulika, kuhifadhiwa na kusherehekewa.

Alisema matukio ya namna hiyo yatasaidia kuenzi, kuishi na kujirithisha falsafa ya Baba wa Taifa ambayo ni urithi na nguzo ya taifa ikiwa katika masuala yanayohusu maadili ya uongozi, muungano, dini, ukabila, na mapambano dhidi ya ujinga, maradhi na umaskini.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, alisema ofisi yake itaendelea kuhakikisha jukumu la ustawi wa viongozi wote waliostaafu akiwamo Maria Nyerere unaangaliwa vyema.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla alisema isingekuwa misingi imara aliyoiweka Hayati Mwalimu Nyerere ambayo ni amani, utulivu na kujitegemea basi wasingekuwapo hapo.

Anna Mwansasu ambaye amewahi kufanya kazi Ikulu na Butiama kwa Hayati Mwalimu Nyerere, alisema kabla ya kifo cha Hayati Mwalimu Nyerere alipata bahati ya kwenda jijini London, Uingereza kumjulia hali na alipofika alimkuta Maria Nyerere anafuma.

"Nilipofika hospitalini Mwalimu Nyerere akaniambia: "Ninaumwa wameniambia itabidi waniongezee damu lakini wakiniongezea damu si itakuwa ya mzungu. Wakiniongezea si nitakuwa siyo Kambarage tena? Pamoja na maumivu aliyokuwa nayo Mwalimu aliongea kwa utani kujitia moyo wa matumaini.".

Makamu Mwenyekiti wa CCM, Abdulrahman Kinana alisema chama kitaendelea kuzingatia misingi imara aliyowaachia Hayati Mwalimu Nyerere.

Waziri Mkuu Mstaafu, Jaji Joseph Warioba alisema Hayati Mwalimu Nyerere alipenda dini lakini alikwepa kuingiza siasa ndani yake, alikuwa mwadilifu, mwenye nidhamu ya hali ya juu, alikuwa na uongozi jumuishi na alipenda kusikiliza.

Mtoto wa Baba wa Taifa, Makongoro Nyerere ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Manyara alisema: "Ninashukuru nimezaliwa na wazazi wema mmoja ametangulia mbele ya haki na mwingine bado yupo."

Alisema: "Mgeni rasmi umezaliwa na wazazi wema Rais Mstaafu ni mtu mwema (Rais wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi), ukiangalia mambo yako yamenyooka ila yangu yana mauzauza, huku ukubwani kuna marafiki tunakutana nao si watu wazuri. Ukiniona ninamauzauza siyo ya Mwalimu Nyerere ni yangu mwenyewe".

Katika sherehe hizo Mama Nyerere alitoa zawadi ya mbuzi kwa viongozi watano ambao ni Rais Samia, Rais Dk. Mwinyi, Majaliwa, Kinana na Majenerali wawili (Kidata na Kalembo) mbuzi mmoja.

# Kigogo wa PAC ashtuka madudu ripoti ya CAG

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WAKATI ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21 ikiendelea kuchambuliwa na wadau mbalimbali, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, amebainisha kushtushwa na mwenendo wa fedha na amana zilizoko kwenye benki za nje ya nchi.

Ripoti hiyo ya CAG iliwasilishwa bungeni jijini hapa Jumanne ya wiki iliyopita na hivyo kuwa wazi kwa umma kwa mujibu wa Katiba.

Katika mazungumzo mahususi na Nipashe jijini hapa jana, Kaboyoka alisema Ripoti ya CAG imeibua 'madudu' mengi na makubwa kwenye mashirika ya umma na taasisi za serikali.

Kigogo huyo wa PAC alipoulizwa na Nipashe kuhusu jambo kubwa zaidi lililomshtua katika ripoti hiyo, alilitaja kuwa ni kushindwa kurudisha fedha na amana zilizo kwenye akaunti za benki za nje ya nchi.

Alitolea mfano Shirika la Bima la Taifa ambalo alisema kwa zaidi ya miaka mitano limeshindwa kufanya miamala kwenye akaunti ya Dola za Marekani Na.11156195 yenye Dola za Marekani 309,800.86, sawa na Sh. milioni 712; na akaunti ya paundi ya Uingereza Na. 0954391 ambapo pesa zake hazikujulikani ni kiasi gani.

Kaboyoka ambaye pia ni Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), alisema akaunti zote hizo ziko katika Benki ya Lloyd jijini London.

"Pili, Shirika la Bandari linamiliki Amana za kudumu zenye thamani ya Sh. milioni 432 huko Benki ya Deutsch, Uholanzi. Haijulikani tarehe ya akaunti kuiva na pesa kulipwa, hivyo rahisi pesa hizo kuingia kwenye hatari ya kupotea," alisema.

Kaboyoka alisema CAG pia amefanya kazi ya ziada kuangalia maeneo mbalimbali yenye matumizi mabaya ya fedha za umma.

MUDA PAC, LAAC

"Ushauri wangu ni kwamba kamati zetu za PAC na LAAC (Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa) zitengewe muda mrefu wa kupitia na kujadili taarifa hii ya CAG ili tuweze kulishauri vizuri Bunge litoe maazimio yatakayokidhi kiu ya walipakodi.

"Kama kamati tajwa hapo juu hazitaweza kupitia sehemu kubwa ya Ripoti ya CAG, kazi aliyofanya hatutaitendea haki maana Bunge ndilo lenye wajibu wa kuisimamia na kuiwajibisha serkali," alisema.

Akizungumza na Nipashe kwenye viwanja vya Bunge jana mchana, Makamu Mwenyekiti wa PAC, Japhet Hasunga, aliunga mkono hoja ya 'bosi' wake kwamba kamati hizo zinapaswa kutengewa muda mrefu zaidi wa kuichambua Ripoti ya CAG.

"Kamati zinapaswa kuichambua ripoti ya jumla kisha zianze kuchambua taarifa zilizopo kwenye ripoti za kisekta. Kwa utaratibu wa kamati kupewa wiki mbili kufanya kazi hii, itakuwa ngumu kuifanya kwa ufanisi," alisema.

Kwa mujibu wa CAG Charles Kichere, taarifa ya ukaguzi wake kwa mwaka 2020/21 ina ripoti 20 zikiwamo zinazohusu hesabu za: Serikali kuu; serikali za mitaa; ukaguzi wa ufanisi; miradi ya maendeleo; mifumo ya Tehama serikalini; mashirika ya umma; haki jinai; na ukaguzi maalum uliofanywa katika maeneo mbalimbali.

# Biteko aanika ukweli jiwe la rubi Dubai

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAPYA yameibuka kuhusu jiwe la Rubi linalotajwa kutokea nchini Tanzania lenye kilogramu 2.8 linalotarajiwa kupigwa mnada Dubai ikiwamo baadhi ya nyaraka kuwa na mkanganyiko zikionyesha kuwapo na mawe mengi zaidi.

Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko (pichani), alitoa ufafanuzi huo jana katika semina ya wabunge ya kuwajengea uwezo kuhusu fursa zilizopo kwenye sekta ya Madini iliyoandaliwa na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO).

Alisema Aprili 13, mwaka huu, walipata taarifa kuhusu jiwe hilo na walikwenda kuangalia kwenye taarifa zao za usafirishaji wa rubi lakini hawakuona hilo jiwe.

"Tukawatafuta wahusika SJ ya Dubai tukawauliza tunaomba kujua hili jiwe kawauzia nani kutoka Tanzania kwa sababu linaonekana limetoka Tanzania limekwenda Dubai, mara ya kwanza kwepa zikawa nyingi kama kawaida tukawaambia sasa kama serikali tunataka kutoa taarifa ndiyo wakatoa taarifa juu ya hili jiwe .

"Wakatuambia kwamba hili jiwe halikutoka Tanzania bali limetoka Marekani. Marekani nani kaliuza, wakatuambia muuzaji anaitwa fulani sitaki kumtaja kwa sababu bado tupo kwenye vikao tunaendelea.

"Tukatuma maofisa wetu wa ubalozi wakaenda SJ wakafanya vikao, kikao cha kwanza kikaja na mapendekezo, ni kweli hilo jiwe limetoka Marekani. Lakini limetoka Tanzania, yule Mmarekani kalitoa Tanzania," alisema.

Alisema wakahitaji nyaraka kutoka kwa huyo Mmarekani kwa kuwa ili kusafirisha madini lazima uwe na cheti halisia na kibali cha kusafirisha kutoka kwenye nchi nyingine.

"Kule wakatuletea certificate ya GIA ya Marekani lakini tukakuta hiyo 'certificate' yenyewe ina matatizo, jiwe limetangazwa lina kilo 2.8 lakini certificate waliyotuletea ina kilo 3.4 tukawaambia mbona hii 'certificate' ni ya Marekani tuleteeni inayotoka Tanzania.

"Wakasema sisi bwana hiyo ya Tanzania hatuna jana tukakubaliana kufanya kikao Ijumaa Marekani, watu wa SJ Dubai ,ubalozi wetu, sisi pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilipofika mchana wakatuomba tuwape muda wakusanye taarifa zaidi,"alisema na kubainisha kwamba wamewaambia si jiwe hilo wana mawe 12 yametoka Tanzania.

"Tukawaambia basi haina shida mliyapata lini? wakasema hayo mawe waliyapata miaka 11 iliyopita. Sasa leo asubuhi kwa sababu tumewaambia tunataka kufanya press wametuletea 'bureau of sell' badala ya mawe 12 kama walivyosema yapo mawe 25 yenye uzito tofauti tofauti,"alisema.

Biteko alisema kunahitajika utulivu kama taifa kwa kuwa haijulikani dhamira yao ni nini ya kutumia jina la Tanzania kwenye biashara ambayo serikali haifahamu.

"Uungwana ilikuwa hivi sisi kama nchi ambao tume export hata kabla hujasema unataka kufanya mnada na ukakubali limetoka Tanzania basi walau tu uwe unawasiliana na yule ambaye ndio mmiliki origin ambako jiwe linapotokea."

"Duniani hapa Wabunge madini yana miiko yake yale yanayoingia kwenye masoko ya kimataifa ni yale tu yaliyokidhi vigezo, kigezo cha kwanza ni lazima yatoke kwenye nchi ambayo haina mapigano ya aina yeyote,"alisema.

Alisema kigezo cha pili madini hayo yachimbwe bila kuvunja haki za binadamu na yaaminike.

"Ukisema jiwe hilo limetoka Tanzania kwanza ni nchi ambayo haina mapigano hilo linakuwa salama kwenye masuala ya kimataifa. Kwa hiyo hatujajua dhamira yao ni nini ndio maana tunatamani utulivu uendelee kuwepo achilia mbali kusema Waziri afanye hiki au hiki ni muhimu watanzania wawe na uchungu na mali yao,"alisema.



"Gem Society duniani wale wanaoshughulika na madini yote ya gemology wametoa tangazo kwa kutoa tahadhari kwa wanunuzi kuwa makini na hilo jiwe. Hilo jiwe ni rubi yenye 'zero site' wanasema limetoka Winza, jiolojia haikubali kwa kuwa rubi ya Winza haina 'zero site', yenye 'zero site' iko Mundalala.

Na pale Mundalala kuna mawe ya aina hiyo mengi mchimbaji mmoja tu anaitwa Sendeu wa Mundalala anayo yale mawe tumeyafunga kwenye kontena na kuyafunga ni tani 8.4. Leo unakuja kuzungumza kilo 2.8 kwa bei ile ni jambo ambalo bado lipo subject to discussion," alisema.

Aliwaomba Wabunge na Watanzania kuwa watulivu taarifa itakapokamilika watatoa maelezo yenye pande zote mbili.

"Tutatoa nyaraka tutatoa vithibitisho kwa sasa kusema jiwe la nani sijui la nani nadhani ni muhimu taarifa mwishoni itaonyesha ni la nani na mambo gani yapo nyuma yake ili Tanzania tubaki kuwa salama. Nitakuwa Waziri wa ajabu sana kama nitakwenda kulichukua option ambayo baadhi wameitoa kwamba watu wamesema nyie mkubali tutumie jina lenu tutawapa Dola milioni 20.

"Mnatupa Dola milioni 20 kwa kipi tunataka tujue hili jiwe limetoka wapi hiki ni kitu cha msingi halafu mambo mengine yatakuja," alisisitiza.

# Wanandoa wafariki dunia usiku chanzo chadaiwa jiko la mkaa

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WANANDOA wawili wakazi wa Mtaa wa Bunkango, Kata ya Nshambya, Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, wamekutwa wamefariki dunia usiku katika nyumba waliyokuwa wakiishi, huku chanzo kikitajwa kuwa ni jiko la mkaa.

Wanandoa hao majina yao hayakupatikana, lakini mtaani wanajulikana kwa majina ya Mama Oswad na Baba Oswad.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Mtaa wa Bunkango, Anath Abas, alisema alipata taarifa kuwa mtoto wa wanandoa hao anayesoma darasa la pili ameshindwa kwenda shule baada ya kugonga mlango wa chumba walimokuwa wamelala wazazi wake kwa muda mrefu bila mafanikio.

Alisema baada ya kupata taarifa hiyo alikwenda eneo la tukio na alipogonga mlango haukufunguliwa, hata alipopaza sauti ya kuwaita hakuna aliyeitika.

Abas alisema baada ya hali hiyo ikamlazimu kuchungulia chini na kumuona Mama Osward amelala chini sakafuni huku mume wake akiwa amelala kitandani.

Alisema aliamua kuwaita viongozi wenzake pamoja na baadhi ya wananchi ndipo wakasukuma mlango na kuingia ndani na kukuta tayari wanandoa hao wamepoteza maisha.

Akizungumzia tukio hilo Diwani wa Nshambya na Meya wa Manispaa ya Bukoba, Godson Gibson, alisema baada ya kupata taarifa hizo kutoka kwa Mtendaji wa Kata alitoa taarifa polisi kwa hatua zaidi, huku akiwaasa wananchi kuacha tabia ya kulala na jiko la mkaa ndani ya nyumba.

"Kuna taarifa kwamba mwanamke alirejea nyumbani usiku akawasha jiko la mkaa na kumenya ndizi, na kisha kuingiza jiko hilo kwenye chumba kisha wakafunga mlango na madirisha," alisema Gibson.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Maketi Msangi amekiri kutokea kwa tukio hilo na kwamba uchunguzi wa awali umeonyesha kuwa vifo vya wanandoa hao vimetokana na jiko la mkaa lililowashwa na kuingizwa katika chumba walimokuwa wamelala.

Alisema: "Uchunguzi wa awali umeonyesha vifo vyao vimetokana na kuvuta hewa yenye sumu inayotokana na mkaa, lakini tunasubiri uchunguzi wa kitabibu ili kujiridhisha kama kweli hicho ndiyo chanzo cha vifo, hivyo na baada ya hapo miili ya marehemu itakabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya mazishi".

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO**

**SHERIA YA UMILIKISHAJI WA ARDHI YA MWAKA 1999**

**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**

**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB.NA.MMC/75/P/MKUNDI**

**MMILIKI ALIOANDIKISHWA: THERESIA M, SODOYEKA S.L.P 681, MOROGORO**

**ARDHI: KIWANJA NA.75 KITALU "P" MKUNDI-MANISPAA YA MOROGORO.**

**MUOMBAJI: METHEW SEDOYEKA S.L.P 181 ,MOROGORO**

Taarifa inatolewa kwamba **BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa siku 14 toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti

**HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO** ikionekana, irudishwe kwa **MKURUGEZI WA MANISPAA –MOROGORO S.L.P 166 MOROGORO**

N.Y. MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

Valency HK
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 51 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late ZIPORA PETRO MGUYE**

**By 1. PETER DEDAN MUNDO**
**2. ………………………………………………**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 05 day of **05….. 2022**
**Dated at MOROGORO this 22 day of 04…2022**

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ELINATHAN B. MAGEMBE** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 562 DGW.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya Polisi: **DAR/MAG/RB/119122/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO**

**SHERIA YA UMILIKISHAJI WA ARDHI YA MWAKA 1999**

**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**

**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB.NA.MMC/LD/3318/3/AM**

**MMILIKI ALIOANDIKISHWA: HAPPINES SODOYEKA S.L.P 681 ,MOROGORO**

**ARDHI: KIWANJA NA.70 &72 KITALU "P" MKUNDI-MANISPAA YA MOROGORO.**

**MUOMBAJI: METHEW SEDOYEKA S.L.P 181 ,MOROGORO**

Taarifa inatolewa kwamba **BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa siku 14 toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti

**HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO** ikionekana, irudishwe kwa **MKURUGEZI WA MANISPAA –MOROGORO S.L.P 166 MOROGORO**

N.Y. MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

Valency HK
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO**

**SHERIA YA UMILIKISHAJI WA ARDHI YA MWAKA 1999**

**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**

**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB.NA.MMC/73/P/MKUNDI**

**MMILIKI ALIOANDIKISHWA: JOSEPH GILUGODA SEDOYEKA S.L.P 681 ,MOROGORO**

**ARDHI: KIWANJA NA.73 KITALU "P" MKUNDI-MANISPAA YA MOROGORO.**

**MUOMBAJI: METHEW SEDOYEKA S.L.P 181 ,MOROGORO**

Taarifa inatolewa kwamba **BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa siku 14 toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti

**HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO** ikionekana, irudishwe kwa **MKURUGEZI WA MANISPAA –MOROGORO S.L.P 166 MOROGORO**

Valency HK
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO….28……2022**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE PASCAL NTIWALE GEDI of NKHUNGU Within DODOMA REGION**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR PROBATE BY KULUTHUMU BAKARI MAGURU**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **25 Day of APRIL 2022**

**Dated at Dodoma this 17TH Day of DECEMBERY 2022**

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO**

**SHERIA YA UMILIKISHAJI WA ARDHI YA MWAKA 1999**

**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**

**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB.NA.MMC/3279/1/AM**

**MMILIKI ALIOANDIKISHWA: MAGDALENA SEDOYEKA S.L.P 681 ,MOROGORO**

**ARDHI: KIWANJA NA.74&76 KITALU "P" MKUNDI-MANISPAA YA MOROGORO.**

**MUOMBAJI: METHEW SEDOYEKA S.L.P 181 ,MOROGORO**

Taarifa inatolewa kwamba **BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa NAKALA HALISI YA **BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa siku 14 toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti

**HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO** ikionekana, irudishwe kwa **MKURUGEZI WA MANISPAA –MOROGORO S.L.P 166 MOROGORO**

Valency HK
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

# Tanzania kumwagiwa mabilioni ujenzi SGR

**Na Benny Mwaipaja,**
WASHINGTON DC

BENKI ya Standard Chartered imeihakikishia Tanzania kuwa iko tayari kutoa fedha zaidi kwenye miradi ya kimkakati inayotekelezwa na serikali ikiwamo ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege.

Ahadi hiyo imetolewa na uongozi wa benki hiyo ukiongozwa na Mwenyekiti wake, Jose Vinals, ulipokutana na kufanya mazungumzo na ujumbe wa Tanzania, ukiongozwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Lameck Nchemba kando ya mikutano ya majira ya kipupwe ya Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), inayofanyika Jijini Washington DC, Marekani.

Akizungumza baada ya kikao hicho kilichofanyika katika Ofisi za Ubalozi wa Tanzania, Washington DC, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba alisema benki hiyo ilitoa mkopo unaotumika kujenga SGR kutoka Morogoro hadi Makutupora mkoani Singida na kwamba hivi sasa serikali iko kwenye mazungumzo na benki hiyo ili itoe mkopo mwingine kwa ajili ya vipande vingine vya reli hiyo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Saada Mkuya Salum, alisema katika kuimarisha shughuli za utalii na kukuza uchumi, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imepanga kuboresha miundombinu ya Uwanja wa Ndege wa Pemba na kwamba mazungumzo yanayoendelea kati ya serikali na benki hiyo yatawezesha kupata fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

Akizungumza kwa niaba ya uongozi wa Standard Chartered, Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo Tanzania, Sanjay Rughani, alisema wako tayari kutoa fedha zaidi kwa ajili ya miradi iliyowasilishwa na Serikali kwenye benki hiyo.

Alisema pamoja na ahadi ya kutoa fedha kwa ajili ya kuendeleza miradi ya kimkakati inayotekelezwa na serikali, benki hiyo pia iko tayari kuwashawishi wawekezaji wengine kutoka maeneo mbalimbali duniani kwenda kuwekeza mitaji na teknolojia nchini Tanzania.

Februari 13, mwaka 2020 Benki ya Standard Chartered, iliipatia Tanzania mkopo wenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa SGR kipande cha Morogoro hadi Makutupora.




Askofu Mkuu mteule wa Kanisa la Mlima wa Moto, Mikocheni, Rose Mgetta, akiongoza maandamano ya kwenda kusimikwa katika kanisa hilo, Mikocheni, mkoani Dar es Salaam jana. Askofu Mgetta anachukua nafasi ya Mwanzilishi wa kanisa hilo, Hayati Dk. Getrude Rwakatare aliyefariki mwaka 2020. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Gwajima alaani mtoto kuuawa kwa maji moto

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amelaani tukio la mtoto Joseph Juma (4) kuuawa na bibi yake, Tatu Moshi (45) kwa kumwagiwa maji ya moto.

Waziri Gwajima alitoa kauli hiyo jana alipofanya ziara mkoani hapa na kutembelea kaburi alilozikwa mtoto huyo nyumbani kwao katika Kijiji cha Lyabukande.

Alisema amelazimika kufanya ziara hiyo mkoani Shinyanga, baada ya kusikia tukio hilo la kuuawa kwa mtoto huyo pamoja na mdogo wake Limmy Lameck (1) kujeruhiwa kwa kipigo na bibi yao.

Waziri Gwajima aliitaka jamii inapoona au kusikia mtoto wa jirani anafanyiwa vitendo vya ukatili, kutoa taarifa haraka ili kudhibiti matukio hayo.

Alisema Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 iliyofanyiwa marekebisho (2019) inakataza mzazi kumuadhibu mtoto na kumsababishia madhara kwenye mwili wake.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alisema katika uchunguzi walioufanya walibaini watoto hao walikuwa wakifungiwa ndani kila siku, wakati bibi na mama yao wanapokwenda kutafuta riziki, lakini majirani walikuwa hawatoi taarifa.

Alisema Serikali mkoani humo wanafanya utaratibu wa kutafuta mlezi ambaye atamlea mtoto huyo kwa muda, wakati mama yake akiendelea kushikiliwa na Jeshi la Polisi, huku bibi yao akishtakiwa kwa tuhuma za mauaji.

Ofisa Maendeleo ya Jamii mkoani Shinyanga, Tedson Ngwale alisema kuanzia mwaka 2021 hadi Machi 2022, matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto yaliyoripotiwa yalikuwa 3,288.

Tukio hilo la mauaji ya mtoto huyo pamoja na mdogo wake kujeruhiwa kwa kipigo na bibi yao, lilitokea Aprili 18, mwaka huu majira ya saa 11 alfajiri.

Baada ya tukio hilo, bibi huyo anashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga pamoja na mama yao, Helena Nicolaus.

## Wataka kuiga mbinu ya Comoro kumaliza malaria

**Na Faustine Feliciane**

WADAU wa afya nchini wameiomba Serikali kuiga mbinu iliyotumika kutokomeza ugonjwa wa malaria katika nchi ya Comoro na Papua Guinea.

Ombi hilo limetolewa wakati dunia ikijiandaa kuadhimisha Siku ya Malaria Duniani Aprili 25, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Saalam, Mtaalamu wa Afya anayefanya kazi na taasisi inayosambaza dawa hiyo kwa nchi za Afrika, Joshua Mwakamela, alisema kwa kuiga kile kilichofanyika katika nchi hizo kunaweza kusaidia kupunguza ama kutokomeza maambukizi ya ugonjwa wa malaria.

Alisema mwaka 2008 na 2007 nchi hizo ziligawa dozi ya Artiquine ambayo ni mchanganyiko wa Artemisinin na Piperaquine iliyotengenezwa na Chuo cha Afya Guangzhou na kusaidia kushusha kiwango cha maambukizi ya ugonjwa huo katika nchi hizo katika kipindi cha miaka mitatu tangu walipogawa dozi hiyo.

"Huu mfumo wa kugawa dozi kwa watu wote kwa kiingereza unaitwa 'Mass drug Administration' ni mpango ambao unatoa dawa kwa wananchi wote. Serikali inaweza kufanya hivyo kwa awamu kutokana na ukubwa wa nchi yetu baada ya muda tunaweza kuona matokeo chanya kama ambavyo imetokea Comoro," alisema Mwakamela.

Alisema wanafanya kazi na Wizara ya Afya na kumekuwapo na ushirikiano mkubwa na ubalozi wa China nchini.

Alisema Serikali imekuwa ikifanya jitihada na juhudi za kutokomeza malaria hapa nchini, hivyo wadau wanapaswa kuisaidia na kushirikiana nao kufikia lengo hilo.

Mbali na Comoro, alisema China imefanikiwa kutokomeza malaria kwa kutumia mtindo wa matumizi ya dawa mbadala 'Traditional Chinese Medicine' (TCM) na kwamba dawa ya Artiquine ndiyo iliyotumika.

Daktari kutoka Hospitali ya Mwananyamala, Dk. Lectin Moris alisema dawa hiyo imefanikiwa baada ya utafiti kufanyika na kuleta matokeo chanya.

Alisema China ilibadili dawa hizo za asili na kuziweka katika mfumo wa vidonge na baada ya kufanikiwa wameanza kuzisambaza Afrika, kwamba nchi za Comoro na Papua Guinea zimefanikiwa kutokomeza ugonjwa huo kwa asilimia kubwa.

HABARI KITAIFA

# Milioni 509/- zatumika kukamilisha mradi wa maji

**Na Happy Severine,** MASWA

MAMLAKA ya Maji na Usafi wa Mazingira Maswa (MAUWASA) imetumia Sh. milioni 509.8 kukamilisha mradi wa usambazaji wa maji katika mji huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa MAUWASA, Mhandisi Nandi Mathias, aliyasema hayo alipotembelea mji wa Maswa kuona utekelezaji wa mradi huo ambao kwa sasa umekamilika na wananchi wameshaanza kupata huduma ya maji safi na salama.

Alisema mradi huo unajulikana kama uboreshaji huduma ya maji Maswa Mjini kwa ustawi wa Taifa kwa maendeleo katika kupambana na maambukizi ya UVIKO-19.

"Fedha za kutekeleza mradi huu zinatokana na fedha za Uviko- 19 ambazo tulizipata kutoka Wizara ya Maji ikiwa ni sehemu ya fedha ambazo Rais Samia Suluhu Hassan alipewa kwa ajili ya mapambano dhidi ya ugonjwa huo," alisema.

Mhandisi Mathias alisema kazi zilizofanyika kwenye mradi huo ni pamoja na uchimbaji wa mtaro na kulaza mabomba kufikia urefu wa kilomita 21.65, ujenzi wa vituo vinne vya kuchotea maji, pamoja na ujenzi wa chemba 10.

Aliongeza kwamba mradi huo umeshakamilika na kwamba umeongeza wigo wa mamlaka hiyo kusambaza maji kutoka asilimia 70 hadi asilimia 80, sambamba na kupata wateja wapya 1,000 na kunufaisha mitaa 10 ya Mjini Maswa.

Mathias aliitaja mitaa hiyo ni Miti Mirefu, Majengo, Sola Mwabomba, Sola, Unyanyembe, Uzunguni, Ujenzi, Jashimba, Ikungulyasubi, Majebele na Badabada. Pia alivitaja vijiji vilivyonufaika na mradi huo ni Iyogelo, Buyubi na Matalambuli.

"Tunaishukuru serikali kwa kutuletea maji katika eneo letu kwani tangu tupate uhuru hatujawahi kuwa na maji safi na salama, hivyo ni jambo la kuishukuru serikali,"alisema Eva Senga, mkazi wa Kijiji cha Iyogelo.

Mkazi mwingine kutoka kijiji cha Buyubi, Grace Khija alisema siku za nyuma kabla ya mradi huo kuanza kufanya kazi walikuwa wakitumia muda mrefu kutafuta maji ambayo walikuwa wakiyapata kwenye mapango ya milima yaliyoko kilomita nane kutoka kwenye kijiji hicho.



Katibuwa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Tawi la Kawawa, Madale, Kata ya Wazo, Wilaya ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, Hadija Mmbaga (kulia), akisimamia uchaguziwa viongozi wa shina namba 8 katika tawi hilo jana, ambapo Mussa Mungoya, alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa shina hilo. **PICHA: JOHN BADI**

# Chongolo ataka jengo machinga kuwa mfano

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo amesema ujenzi wa eneo maalum la wafanyabiashara wadogo katika Jiji la Dodoma uwe darasa la mfano kwa mikoa mingine, ili wafanye biashara zao kwenye mazingira mazuri na yenye hadhi.

Aliyasema hayo jana alipokuwa akizindua shina la wakereketwa wa madereva bodaboda na bajaji Kilimani jijini hapa.

Alisema Jiji hilo linatumia Sh.bilioni 7.5 kwa ajili ya kujenga eneo hilo ambalo litatatua kero ya wafanyabiashara wadogo.

"Nipongeze uongozi wa Mkoa wa Dodoma na Jiji la Dodoma kwa kazi kubwa mnayoendelea kuifanya. Nimepita pale siyo zaidi ya mara mbili, mara tatu, zaidi ya mara tano na nimefika nikaamua kushuka si mara moja ili kuangalia eneo lile mnalojenga kwa ajili ya machinga, kazi ile mnayoifanya sasa wafanyabiashara watakuwa kwenye eneo lenye heshima na hadhi ya kufanyia biashara,"alisema Chongolo.

Hivyo, alitaka kukiwa na mikutano ya viongozi mkoani Dodoma wanaotoka mikoa mbalimbali wafike kuona eneo hilo kujifunza.

Akizungumza kuhusu shina lililozinduliwa, Chongolo aliwataka vijana hao kulitumia kwa ajili ya kazi, ili kujikwamua kiuchumi na lisiwe kijiwe cha kupiga porojo.

"Mmeanzisha shina lenye lengo la kujikwamua na umaskini. Kikubwa ni sisi kuhangaika kuwawekea mazingira mazuri ili mstawi leo unaendesha bodaboda kesho uendeshe bajaji, keshokutwa uendeshe taxi, hayo ndiyo maendeleo, mtengeneze makazi bora, kusomesha watoto...ndani ya wiki mbili mtapata bodaboda yenu Rais akiwasili nchini," alisema Chongolo. Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alisema pindi watakapokabidhiwa pikipiki hiyo waitunze na waitumie kwa lengo lililopangwa.

Alisema dhamira ni wafanyabiashara wapate sehemu nzuri yenye staha na kuwa na anwani ya maeneo wanayofanyia biashara ili kupata mikopo, kwamba Benki ya NMB imetenga Sh.bilioni mbili kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wafanyabiashara hao.

# RC: Hakuna shule hii mkoani Ruvuma

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, amekanusha taarifa zinazoeleza Shule ya Msingi Litapatile katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba wanafunzi wake wanasoma katika mazingira mabovu.

Hivi karibuni kulikuwapo na video iliyokuwa ikisambaa katika mitandao ya kijamii ikionyesha wanafunzi wa shule hiyo yenye wanafunzi 13 waosoma darasa la tatu wanasoma katika mazingira mabaya yasiyo na miundombinu rafiki na kwamba shule hiyo imejengwa kwa miti.

Akizungumza na waandishi wa habari, Brigedia Jenerali Ibuge alisema hakuna shule inayoitwa Litapatile katika Halmashauri ya Madaba na Mkoa wa Ruvuma, hicho chanzo cha taarifa hiyo ni uzushi.

Alisema msimamo wa serikali ya mkoa ni kwamba watoto hao wanayo haki ya kupata elimu kwa mujibu wa katiba ya nchi na wazazi wanao wajibu wa kuhakikisha watoto hao wanaandikishwa na kuhudhuria masomo kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Brigedia Jenerali Ibuge ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Ruvuma alisema kuwa kibanda hicho kinachotumika kuwafundishia wanafunzi hao kipo umbali wa kilomita kati ya 48 na 50 kutoka Kata ya Mtyangimbole.

Alisema kuwa walichotakiwa kufanya wazazi wa watoto hao ni kuhakikisha shughuli zao haziathiriki, haki ya watoto wao kuandikishwa shule na kupata elimu, hivyo serikali ya Mkoa wa Ruvuma itasimamia haki ya watoto kupata elimu kwa utekelezaji wa Sheria ya Elimu namba 25/1978 inayolinda haki ya mtoto ya kupatiwa elimu.

Alisema pia ni kosa kwa mzazi kutohakikisha kuwa mtoto wake anaendelea na shule hadi kufikia darasa la saba, kwamba mtu yoyote atakayesababisha mtoto wake asiendelee na masomo atashtakiwa.

Alisema serikali ya mkoa haitamvumilia mzazi yoyote atakayemnyima mtoto haki ya kwenda shule kwa makusudi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Viongozi wazingatie sheria, miiko katika kutoa matamko

KATIKATI ya wiki hii, madereva wa bajaji na bodaboda mkoani Dar es Salaam, waliandamana hadi ofisi ya Mkuu wa Mkoa, ikiwa ni hatua ya kupinga zuio lililowekwa la kufanya shughuli za usafiri katikati ya jiji wakiwa na abiria.

Zuio hilo lilitangazwa na Jiji la Dar es Salaam, hivyo kusababisha madereva hao kuandamana na matokeo yake kuibua taharuki kwa wananchi ikiwamo kusababisha kufungwa kwa Barabara za Kawawa na Uhuru.

Hatua hiyo ilisababisha viongozi katika jiji akiwamo Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ngw'ilabuzu Ludigija, kuwatuliza madereva hao kwa kile alichosema uongozi, ikiwamo ofisi ya Mkuu wa Mkoa imepokea kilio chao. Baada ya kuelezwa hivyo, walikubali kuacha mgomo na hatimaye kufunguliwa kwa barabara iliyokuwa imefungwa.

Sababu kubwa ya kugoma kwao, kwa mujibu wa viongozi wa madereva hao, ni viongozi walio katika mamlaka kushindwa kujali shida zao na kwamba wanapokuwa katika nafasi zao wanatoa matamko bila kujali watu wanaowaongoza wakiwamo wenye ulemavu, hususan madereva hao wa bajaji na bodaboda.

Pamoja na kuchukuliwa kwa hatua hiyo, Waziri mwenye dhamana na tawala za mikoa na serikali za mitaa, Innocent Bashungwa, aliwasiliana na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, kuwa zuio hilo lisitishwe na kufanyika kwa kikao kinachoweza kuleta maelewano baina ya viongozi na madereva hao.

Katazo hilo la Halmashauri ya Jiji kuhusu madereva ni moja ya mambo ambayo yamekuwa yakifanywa na mamlaka za serikali kuu na zile za mitaa juu ya mambo yanayohusisha jamii. Matokeo ya baadhi ya matamko hayo, yamekuwa yakisababisha sintofahamu katika jamii na uvunjifu wa amani.

Mfano mwingine wa matamko kama hayo ni miaka ya karibuni ambapo kiongozi mmoja alitoa amri kwamba abiria katika mabasi ya abiria mkoani Dar es Salaam, maarufu kama daladala, hawatakiwi kusimama ikiwa ni hatua ya kujikinga na ugonjwa wa UVIKO- 19.


Hata hivyo, amri hiyo haikutekelezwa kwa sababu hakuna aliyefuatilia na hata waliopewa dhamana ya kusimamia sheria hawakuona umuhimu wake kwa sababu walijua matokeo yake yangekuwa mabaya.

Kutokana na matamko ya baadhi ya viongozi hao, jamii inachukulia kwamba wamekuwa wakifanya hivyo kwa ajili ya kujipatia umaarufu kisiasa kwani miongoni mwa kauli au maagizo hayo hayazingatii sheria, kanuni na taratibu za kiuongozi.

Umefika wakati kwa viongozi kuacha mihemko ya kisiasa au kutafuta umaarufu kupitia matamko wanayoyatoa ambayo wakati mwingine yanaweza kusababisha maafa katika jamii. Inawezekana baadhi yao wanafanya hivyo kwa kutokujua miiko ya uongozi au wanapaswa kufanya nini wanapokuwa katika nafasi zao za uongozi.

Tunadhani, kuna umuhimu wa namna yake kwa viongozi hawa wa kisiasa, kabla ya kushika nafasi wanazoteuliwa na mamlaka za juu, wapelekwe katika mafunzo ya muda mfupi, zikiwamo semina elekezi ili kunolewa juu ya wajibu wao. Tunaamini kwamba kwa kufanya hivyo watajua miiko na taratibu pamoja na mipaka ya majukumu yao katika utekelezaji wa kazi zao za kila siku.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Figisu hizi ni hatari kwa demokrasia ndani ya CCM



Na Sabato Kasika

**MWAKA** huu Chama Cha Mapinduzi (CCM), kinafanya uchaguzi wa viongozi wake, na tayari kimeanza mchakato huo kwenye ngazi ya mashina ambapo wanachama wanaendelea kuchagua viongozi wao.

Hata hivyo, wakati mchakato huo unaendelea, kumeibuka figusi ambazo zimesababisha Katibu Mkuu wa chama hicho Daniel Chongolo kuingilia kuagiza utoaji wa fomu za kuwania uongozi urudiwe upya kwenye baadhi ya maeneo.

Katibu huyo amechukua uamuzi huo kufuatia kuwapo kwa madai kwamba, baadhi ya makada wa chama hicho wamenyimwa kwa makusudi fomu za kuwania uongozi ili wasipate fursa hiyo.

Baadhi ya maeneo ambayo kiongozi huyo ametoa maelekezo ya kugawa fomu upya ni Wilaya ya Ubungo na Kinondoni mkoani Dar es Salaam, wakati akizungumza na Halmashauri Kuu za wilaya hizo.

Anataja maeneo kama Tandika, Manzese, Kimara, baadhi ya makatibu wa matawi kwa sababu wana maslahi yao binafsi wanawanyima baadhi ya wanachama kuchukua fomu kwa kuwaambia fomu zimeisha na hawawapatii ili wawapitishe watu ambao wanafikiri watasimamia maslahi yao.

Lakini pia anawaagiza makatibu wa wilaya zote nchini na maeneo yote ambayo wamebaini kuna matatizo hayo mchakato huo urudiwe kwa lengo la kuhakikisha kila mwanachama mwenye nia ya kuwania uongozi asibaniwe.

Nionavyo ni kwamba, hatua alizochukua Katibu Mkuu huyo ni sahihi, kutokana na ukweli kwamba, figisu kama hizo zinaweza kuhatarisha demokrasia ndani ya chama hicho kikongwe.

Chongolo anakumbusha kuwa katiba ya chama inatoa fursa na haki kwa kila mwanachama kuchagua na kuchaguliwa, lakini anasikitika kuona baadhi ya maeneo, wanachama wananyimwa fursa hiyo kwa makusudi. Kwa kuwa kila mwanachama ana haki ya kuwania uongozi ili mradi awe anatimiza vigezo vinavyotakiwa, ninadhani hakuna haja ya kuwawekea mizengwe au figisu, hali ambayo inaweza kupasua chama.

CCM ni chama kikongwe, hivyo ni vyema viongozi wake wawe mstari wa mbele kusimamia demokrasia ili kuwa mfano bora kwa vyama vingine visipate upenyo wa kukikosoa mbele ya umma.

Ikumbukwe kuwa chama hicho si cha mtu binafsi au cha kikundi fulani, bali ni cha wanachama wote, ambao kila mmoja ana haki kuwania uongozi, hivyo ni wazi kwamba waliowanyima fomu wenzao, watakuwa wameteleza. Mtindo huo wa kuwekeana mizengwe ndiyo ambao umekuwa ukilalamikiwa na baadhi ya vyama vya upinzani unapofanyika mchakato wa uchaguzi unaojumuisha vyama vyote vya siasa. Ninadhani umefika wakati sasa wanasiasa kuachana na mtindo wa kutafuta ushindi wa mezani, badala yake wachukuane ili mshindi apatikane kihalali badala ya kupatikana kwa njia ya mkato.

Pamoja na hayo, Katibu Mkuu anaweka wazi kuwa chama si cha mtu, bali ni cha wanachama wote, hivyo wale waliofanya mchezo wa kuficha fomu ni vyema wangetanguliza maslahi ya chama kwa kuhakikisha kila mgombea anapata fomu.

Ninaamini kuwa mtindo wa kuwekeana vigingi au vizuizi, katika kuwania uongozi, unajenga chuki na matabaka ndani ya chama na hatima yake inaweza kuwa ni baadhi ya makada kukisaliti chama.

Lakini pia hatua zilizochukuliwa na Katibu Mkuu huyo za kuagiza fomu kutolewa upya, zingekuwa ni funzo kwa makatibu wa matawi ambao inadaiwa kuwa kwa maslahi yao binafsi wamewanyima fomu baadhi ya wagombea.

Kimsingi ni kwamba, mchakato wa uchaguzi ukifanyika kwa mujibu wa katiba, sheria, kanuni na taratibu za chama, kuna uwezekano mkubwa wa kupata viongozi wanaokubalika kwa wanachama wote.

Hivyo ni wazi inapokuwapo mizengwe kama hiyo inayodaiwa kufanyika ndani ya chama hicho, ni wazi wanaochaguliwa ni wale wasio chaguo la wanachama bali ni kwa maslahi ya viongozi wachache.

Ni vyema viongozi waliowanyima fomu baadhi ya wagombea walifanya hivyo kwa lengo gani, kwani wanaweza kuwa wanataka wawalindie maslahi yao, hatua ambayo kimsingi haina afya kwa chama.

Mtindo wa kutafuta ushindi wa mezani au kupita bila kupingwa unaweza kuchangia kupata viongozi wasiofaa, badala yake makada wachuane majukwaani kwa hoja kisha wanachama waamue ni nani anawafaa.

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Tanzania tunaendelea kufanywa kuwa shamba la Bibi hadi lini?



Na Pascal Mayalla

**Naunga mkono uzinduzi wa Royal Tour kufanyikia Marekani. Ni mahali sahihi Kwa sababu huko ndiko kwenye ‘catchment areas’ za watalii wenye fedha. Pia kwa mawazo yangu, kwa vile lengo, pamoja na mambo mengine, ni kuutangaza utalii wetu hususan vivutio vilivyopo ili kuhamasisha watalii wengi zaidi kuitembelea Tanzania, hakuna kitu kinachoongoza kwa kutangaza utalii kama usafiri wa ndege wa moja kwa moja.**

NAENDELEA na makala zangu za “Kwa Maslahi ya Taifa” na leo ni kuhusu uzalendo wa kujitolea kuisaidia serikali yako na nchi yako, pale unapoona imeshindwa na inahitaji msaada. Swali kubwa, je tutaendelea kufanywa shamba la bibi hadi lini?

Hili ni mada ya kuisaidia serikali yetu kuhusu hii rubi. Swali ni Tanzania tutaendelea kufanywa “Shamba la Bibi” hadi lini?. Hii Burj Alhamal Ruby ni yetu, iweje iko sokoni Dubai, lakini serikali yetu haijui chochote?

Uzalendo ni kuipenda nchi yako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote na kwa nafsi yako yote na kuilinda na kuitetea kwa moyo wako wote, kwa nguvu zako zote, na kwa uwezo wako wote. Ikibidi kuipigania, uwe tayari kuutoa uhai wako kuifia nchi yako.

Uzalendo wa kweli hukaa ndani ya mtu, hauonekani kwa macho, bali hukaa moyoni, hivyo kuna watu ukiwaangalia kwa juu juu kwa jinsi wanavyoonekana, wanaonekana kama ni wazalendo, lakini kiukweli si wazalendo kwa lolote wala uzalendo chochote, bali ni wapigaji.

Baadhi yao ndio mafisadi wakubwa. Wamejivisha ngozi ya kondoo ya uzalendo lakini ndani yao ni mbwa mwitu, fisi, chui. Pia kuna watu ni hohehahe, masikini wa kutupwa, wanaoishi kwenye lindi la umasikini uliotopea, lakini ndio wazalendo wa kweli wa taifa lao, na katika kundi hilo, mimi ni mmoja wao.

Ukiona kuna kitu serikali yako imeshindwa na wewe unaweza kusaidia, saidia tu usingoje kuombwa.

Kwenye ulinzi wa rasilimali zetu, kwa muda mrefu Tanzania tumekuwa na kilio cha kufanywa shamba la bibi kwa manyang’au kutuibia kama hazina mwenyewe!

Hivi ninavyoandika hapa, kuna jiwe la kito cha thamani aina ya rubi kutoka mgodi wa Winza kule Dodoma, lenye uzito wa kilo 2.8 ambalo limechimbwa na mchimbaji mdogo, serikali haijui.

Mchimbaji huyo hajui thamani yake hivyo ameuza bei ya kutupa, serikali haijui. Mnunuzi kaliondoa nchini kinyemela serikali haijui. Limeuzwa serikali haijui na mnunuzi kaliuza kwa tajiri wa Kiarabu, serikali haijui. Tajiri wa Kiarabu kalibatiza jina la Burj Alhamal Ruby, serikali haijui.

Sasa Burj Alhamal Ruby liko sokoni Dubai, likisubiri mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhan uishe, lipigwe mnada, serikali haijui!.

Mbunge wa Mkinga, Dunstan Kitandula, anauliza Bungeni kuhusu jiwe hili, Waziri wa Madini anashangaa na yeye kusema serikali haijui ila na wao wamesikia mitandaoni!.

Serikali si mtu ni taasisi, ina jicho kali linaona kila mahali, ina mkono mrefu unafika kila kona, hivyo katika hali ya kawaida, haiwezekani haya yote yatokee Tanzania.

Tutaendelea kufanywa shamba la bibi hadi lini?. Kwa vile sasa tunaishi kwenye ulimwengu wa sayansi na teknolojia, kila kitu ni kwenye ncha za vidole vyako, kuisaidia serikali yetu ipate pa kuanzia, hizi ni data zote za jiwe hili akiwamo mmiliki.

Huyu dogo ndiye mchimbaji wa jiwe na huyu jamaa Steve Ulatowski , ndiye mtaalamu wa madini aliyepima ‘properties’ za jiwe hili, sasa analisagia kunguni ili mnada usifanyike kwa sababu hilo jiwe limepigwa.

Haya kazi kwenu serikali yetu. Anzieni na mchimbaji, ila halahala ‘msimuharasi’ tu.

Kwa mujibu wa mtaalamu wa miamba ya madini, japo hili jiwe la hii rubi limeingizwa soko la kimataifa kwa makaratasi ya kuonyesha limechimbwa mgodi wa Winza, hizo karatasi ni za kughushi, hili jiwe limechimbwa Longido Arusha na mchimbaji mdogo ambaye hajui thamani yake, hivyo alishikishwa kidogo dogo cha pesa mbuzi, kwake akaziona nyingi, jiwe likaondoka Longido.

Ili jiwe liingie katika masoko ya kimataifa, ni lazima lisajiliwe na kupatiwa ‘certificate of origin’, hivyo ukatafutwa mgodi wa rubi ambao uko tayari kutoa hati hiyo na hapo ndipo mgodi Winza ulipoingia ukatoa hati feki mzigo uingie sokoni. Jamaa wakalipwa chao, wakaingia ‘front’ kuwa jiwe ni lao, wakaliandikia hati, na sijui kama kodi za serikali zililipwa ndiyo maana serikali haijui.

Hawa mgodi wa Winza, walifanya kosa moja tuu, walipima uzito bila kupima ‘properties’ na kulisajili kuwa wamelichimba wao.

Hilo jiwe lina ‘properties’ za kitu kinachoitwa ‘zoisite’, ambacho kinapatikana Longido tu, sasa iweje rubi ya ‘zoisite’ ipatikane Dodoma?

Ni kama jiwe la Tanzanite linapatikana Mirerani pekee, lakini muuzaji mkubwa namba moja wa Tanzanite ni India akifuatiwa na Afrika Kusini, Tanzanite inapatikana Mererani pekee nchini Tanzania, hiyo Tanzanite ya India inayoongoza duniani na Afrika Kusini, inatoka wapi?

**Tanzania tunaendelea kufanywa shamba la bibi hadi lini?**
**Wasalaam**
**Paskali**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# CAG kamaliza ngwe yake, tugange kijacho



Na Joseph Kulangwa

**Inatisha lakini tunafanyaje, wananchi ndivyo wanavyoamua ukatili. Lakini baada ya kuangalia hiyo picha kuna baadhi ya watu wakaandika chini yake, wakisema kama huyu mwizi wa kuku tu anafanywa hivi, je wale aliowagundua CAG katika ukaguzi wake wanastahili adhabu gani?**

NIMETAZAMA kibonzo cha mwanamke akiwa na mbwa aliyemfunga kamba akitembea naye, akionekana kutaka kung’ata watu, huku akibwekea watu wawili, mwanamke na mwanamume.

Ubavuni mwa mbwa huyo, kuna maandishi ya CAG na mwenye mbwa huyo kawekewa maneno, kwamba “jamani msiogope huwa anabweka tu, haumi...” Wawili hao wanaonyesha hofu kubwa kwamba mbwa huyo anaweza kuwadhuru. Lakini katika sehemu nyingine pia nikakumbana na picha ya kijana amevishwa gurudumu la gari huku likiwaka moto na watu jirani wakishuhudia na wengine wakiendelea kuuchochea moto huo.

Mara moja kwa kuangalia picha ile, nahitimisha kuwa ni mwizi na hiyo ni adhabu anayopewa na umma wa watu wenye hasira. Huko ndiko kunasemekana kujichukulia sheria mkononi. Inatisha lakini tunafanyaje, wananchi ndivyo wanavyoamua ukatili.

Lakini baada ya kuangalia hiyo picha kuna baadhi ya watu wakaandika chini yake, wakisema kama huyu mwizi wa kuku tu anafanywa hivi, je wale aliowagundua CAG katika ukaguzi wake wanastahili adhabu gani?

Matukio haya mawili yanafikirisha sana, husussan baada ya kusoma taarifa ya CAG yaani Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, aliyoiwasilisha bungeni hivi karibuni ili ijadiliwe.

Ukisoma taarifa ile, hutaamini kwamba uko Tanzania, nchi ambayo katika miaka ulipofanyika ukaguzi huo, ilikuwa ikijinasibu kuwa nchi yenye nidhamu ya matumizi, hata kuchangia kuwa na uchumi wa kati wa chini!

Hutaamini kabisa kuwa ni nchi ambayo ilikuwa sasa inasogelea kuwa kama Ulaya, nchi tajiri kabisa katika Afrika! Nchi ambayo katika kipindi hicho ilijinasibu kurejesha nidhamu katika maeneo mbalimbali ya kazi na utumishi.

CAG katika taarifa yake, kaja kutwambia kuwa hakuna kitu bali ni maneno tu, kwamba kila mahali ni upigaji, ni wizi, ni ufisadi, ni uporaji na ni unyang’anyi wa fedha na mali za Watanzania walipa kodi wanyonge!

Sina uhakika kama CAG katika majukumu yake huwa haruhusiwi kutoa sifa palipofanyika vizuri au yawezekana alishindwa kupaona kutokana na hali ya kugubikwa na mambo kama haya yanayosikitisha.

Kila alipogusa ni madudu, kila alipotazama ni uchafu tu na kila alipoangalia ni takataka kabisa! Ndivyo Tanzania ya mwaka 2020/21 ilivyokuwa? Kweli enzi za Mtetezi wa Wanyonge mpambanaji wa rushwa na unyanyasaji ndivyo hali ilikuwa?

Yaani pamoja na wale wa vyeti feki kuondolewa kazini, pamoja na mishahara hewa kukomeshwa, ndivyo sasa watu walivyoamua kufakamia kilichopatikana na kilichobaki kweli mpaka CAG kuibuka na haya?

Mi naona hata hiyo nidhamu ikirejea ilikuwa ni ya “Karibu mteja tukusaidie nini!” Wala si ile nidhamu ya kuogopa na kuheshimu mali na fedha za umma! Watu walipakwa mafuta kwa mgongo wa chupa na kuaminishwa yasiyokuwapo na ndicho kinachodhihirika leo.

Turudi kwenye ile mifano ya awali ya kikaragosi na picha ya mtu kuchomwa moto. Je, ni kweli mbwa wetu huyu ataishia kubweka tu na kujiondokea? Najua CAG huwa ni kama mpelelezi mahakamani ambaye hupeleleza na kuendesha mashitaka huyo huyo na kumwachia hakimu au jaji aamue.

Kichere kamaliza hatua zake hizo mpaka kufikia hatua ya kumwachia hakimu aone hawa watu walikutwa na kesi ya kujibu sasa wafanywe nini. Kwa hiyo huyo mama aliyeshika kamba ya mbwa, sasa anapaswa kushika fimbo awachape waliobanika kuharibu.

Kwa maana hiyo hiyo, ni kwamba sasa hao aliowabaini Kichere kufanya madudu, ndio sasa wavishwe magurudumu na kutiwa viberiti, ili waipate chungu waliyoisababisha kwa Watanzania kutokana na kupewa dhamana na kushindwa kuzitumikia.

Kwa kweli Chifu Hangaya ana kazi kubwa ya kufanya, akipitia taarifa ya CAG Kichere ukurasa kwa ukurasa, na ili arejeshe imani ya Watanzania kwa Serikali yao, basi kila ukurasa aufanyie kazi na haki ionekane kutendeka.

Watanzania tayari wameshajua kuwa kumbe kuna mchezo unafanyika kupitia maneno mengi ya wanasiasa, kutuaminisha mambo yanakwenda vizuri lakini kumbe ni kutwanga maji kwenye kinu, yakiturukia wenyewe. Hebu kwa hili tuone kazi ikiendelea basi eh!

**Alamsiki!**

# Mahakama 10 za mfano kujengwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIKA mpango mkakati wa awamu ya pili wa maboresho ya mahakama nchini ulioanza 2020 hadi 2025, Mahakama ya Tanzania inatarajia kujenga Mahakama 10 za mwanzo za mfano.

Hayo yalibainishwa jana jijini hapa na Mtendaji Mkuu wa Mahakama Tanzania, Prof. Elisante Ole Gabriel, alipotembelea Kijiji cha Haubi, Kondoa mkoani Dodoma.

Prof. Gabriel alisema kati ya Mahakama hizo, mbili zitajengwa Dodoma katika kijiji cha Kinusi wilaya ya Mpwapwa na nyingine Haubi wilaya ya Kondoa.

Alisema Mahakama inaendelea na maboresho ambapo kwa mujibu wa mpango mkakati ulioanza tangu 2015 hadi 2020 mambo makubwa mengi yamefanyika.

"Hivi sasa tupo katika mpango mkakati wa awamu ya pili,katika mpango mkakati huu kutakuwa na maboresho kwani hadi sasa Tanzania kuna Mahakama za mwanzo 960 huku mahitaji yakiwa ni 3900 hivyo bado kuna upungufu," alisema Prof. Gabriel.

Alisema Jaji Mkuu, Profesa Ibrahim Hamisi Juma katika vikao vyao alielekeza kuwa ni vyema kuangalia namna ya kujenga mahakama za mwanzo kwa kuzingatia maeneo yasiyo pungua 10 ambayo ni vigumu wananchi kufika katika mahakama.

Prof. Gabriel alisema serikali itajenga jengo jipya la Mahakama ya mwanzo na nyumba mbili za Watumishi ambapo wanahitaji ardhi isiyopingua ekari mbili na uhamasishaji wa wananchi ili kuthamini kile kitakachojengwa ikiwemo kujitolea kwa wananchi kushiriki shughuli za ujenzi.

Kwa upande wake Diwani wa Haubi, Paul Irovya, alisema ni kweli mahakama iliyopo ilijengwa muda mrefu kabla ya Uhuru na majengo yake yamechakaa yanahitaji matengenezo au ujenzi rasmi.

Alisema ujenzi wa mahakama yenye hadhi litakuwa jambo jema kwa sababu itawapunguzia wananchi mzigo wa kusafiri umbali mrefu kwa ajili ya kutafuta haki.

"Tunaishukuru serikali kwa maono yake na kuamua kujenga mahakama hapa Haubi, tunaamini itakuwa na tija kwa wananchi wetu kwa sababu itawarahisishia na kuwapunguzia mzigo mkubwa waliokuwa wamebeba wa kusafiri umbali mrefu,"alisema Diwani.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Haubi, Anasi Lubuva, alisema licha ya kuwapo kwa mahakama hiyo iliyochakaa lakini bado kuna changamoto ya kukosa Hakimu kwa kuwa aliyepo anahudumia Mahakama zaidi ya mbili.

Alitaja changamoto nyingine iliyopo katika kijiji hicho kuwa ni Mabaraza ya Kata yaliyopo hayana ujuzi namna ya kuendesha kesi, wakati mwingine wanaendesha kwa uzoefu si kwa kufuata sheria, hivyo ni vyema wakaandaliwa semina maalumu kwa ajili ya kufundishwa namna ya kuendesha kesi.

# Mongella: 'Royal Tour' kuongeza idadi watalii

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, amempongeza Rais Samia Suluhu kwa kuandaa filamu ya "Royal Tour" itakayoleta tija kwa kuongeza idadi ya watalii wa nje ya nchi.

Mongella aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uzinduzi wa filamu ya Royal Tour utakaofanyika Aprili 28 mwaka huu katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa AICC mkoani Arusha.

Alisema utengenezaji wa filamu hiyo ulioanza Zanzibar hadi Tanzania Bara umetoa fursa kubwa za kuutangaza utalii ndani na nje ya nchi.

"Filamu hii kwetu tunafahamu licha ya kuongeza idadi ya watalii pia itaongeza mapato ya nchi na mtu mmoja mmoja, hivyo muhimu kuunga mkono jitihada hizi,"alisema.

Mongella alisema utengenezaji wa filamu hiyo umeainisha mambo mbalimbali ikiwamo machimbo ya madini ya Tanzanite yaliyopo Mirerani pamoja na vivutio vya utalii vilivyopo katika hifadhi mbalimbali kama vile Ngorongoro, Serengeti na Mlima Kilimanjaro.

"Nawaomba wananchi wajitokeze kushuhudia uzinduzi huu utakaofanyika ukumbi wa AICC Aprili 28 mwaka huu, nampongeza Rais Samia kwa kuutangaza utalii wa ndani na nje ya nchi, kwani ni moyo wa kizalendo wa hali ya juu,"alisema.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa ya kuutangaza utalii, hivyo aliwaomba Watanzania wamuunge mkono katika kuinua sekta ya utalii na sekta nyingine.

Pia, aliwaomba wakazi wa Kilimanjaro na Mkoa wa Arusha kujitokeza kwa wingi kumpokea Rais Samia atakapotua Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) Aprili 28 mwaka huu, kwa ajili ya uzinduzi wa filamu hiyo.

Alisema katika uzinduzi huo wanatarajia kuwa na wageni na viongozi mbalimbali wa kitaifa, mabalozi, wawekezaji, wadau wa utalii na uhifadhi, wafanyabiashara pamoja na wananchi kutoka katika mikoa jirani ikiwamo Kilimanjaro, Tanga, Manyara, Mara.

Mongella alisema kwa sasa idadi ya watalii wa ndani wanaotembelea maeneo ya hifadhi imeongezeka kutoka watalii 562,549 mwaka 2020 hadi kufikia watalii 788,933 mwaka 2021.




Makamu wa Rais na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Philip Mpango, akipiga kura katika uchaguzi wa mwenyekiti na wajumbe wa CCM wa Shina Na. 5 kitongoji cha Kihanga, Kijiji cha Kasumo, Buhigwe mkoani Kigoma juzi. **PICHA: OMR**

# Vingunguti wafurahia maji safi kutoka DAWASA

**Na Joseph Mwendapole**

WANANCHI wa Mtaa wa Kombo Kata ya Vingunguti, wameanza kupata huduma ya majisafi na salama ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA).

Akizungumza kwenye mkutano wa wananchi, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Vingunguti, William Kibeyo, aliwaondoa hofu wananchi kuhusu huduma hiyo, huku akiwaeleza kuwa mabadiliko hayo ya uendeshaji wa mradi yanatokana na takwa la kisheria na mabadiliko ya sheria.

Alisema Sheria Namba 5 ya mwaka 2019 inaitaka DAWASA kuhudumia maeneo yote ya kihuduma na shughuli za jumuiya na kamati kukabidhiwa kwenye mamlaka.Kibeyo alisema miundombinu ya maji ya kamati iliyojengwa na Shirika la Maendeleo la Plan International itaunganishwa katika mfumo wa maji wa DAWASA na wananchi wasioweza kumudu gharama za kuunganisha huduma wataendelea kuhudumiwa kupitia kizimba hicho kwa gharama iliyowekwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

"Gharama iliyowekwa na EWURA kwa ndoo ya maji ya lita 20 ni shilingi 50 hii itasaidia familia ambazo bado hazijajipanga vizuri kuomba huduma ya maji katika nyumba zao," alisema.

Meneja wa Mkoa wa Kihuduma DAWASA Tabata, Boniface Ole, alisema: "Utaratibu wa Serikali ni lazima mtumiaji wa maji awe na dira inayoonyesha matumizi yake, hapa wengi walikua hawana dira na kusababisha kutumia huduma ya maji bila kulipia"

Aliongeza: "Awali tulisitisha huduma na kuwasihi wananchi wajitokeze ili wajisajili DAWASA na kutambulika ili wafungiwe dira za maji" Alisema mwitikio ni mzuri kwani kati ya wananchi 100 waliositishiwa huduma, wameweza kuwarudishia wananchi 29 na zoezi linaendelea.

Ole alitoa wito kwa wananchi ambao bado hawajajaza fomu wala kujisajili DAWASA wajitokeze Ili wafungiwe dira za maji na kuendelea kupata huduma kwa haraka.

Mabadiliko ya uendeshaji wa kamati za maji zilizokuwa chini ya halmashauri yamefanyika kufuatia mabadiliko ya Sheria ya Maji namba 5 ya Mwaka 2019 na kwamba miradi yote ya jamii itakabidhiwa katika mamlaka za maji kwa usimamizi na uendeshaji wenye tija.


# MAISHA

APRILI 24, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili

Ukurasa 12

## HARUSI



Ukurasa 13

## Vito; huendana na vazi maalumu



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Tambua athari za kujenga katika udongo wa mfinyanzi




## KOPE ZA ASILI


# Tumia njia hizi utapenda

Ukurasa 14

# WATOTO

MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | S | A | N | D | A |
| ■ | H | ■ | ■ | A | ■ |
| B | A | A | ■ | N | ■ |
| ■ | M | ■ | U | D | A |
| ■ | B | ■ | ■ | I | ■ |
| T | A | M | K | A | ■ |





## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
IGA, UMA, JANGA, JEMBE, BONGEA, JAMBIA




Alichokifanya daktari

MTOTO John alitumwa na mama yake akalete asali kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

Baada ya kuileta mama yake alichukua kidogo na kuilamba mdomoni huku akimwambia John kwamba asali ni tamu sana na inaleta afya kwa binadamu.

**John:** Sawa mama lakini mbona unailamba wakati wewe huna mzinga wala hujui kuutengeneza?

**Mama:** Hapana John kuilamba sio uwe unajua kutengeneza mzinga wa nyuki, bali ni moja ya njia ya kula tu.

**John:** Sasa mama mbona mwalimu katuambia ukilamba asali mwishowe utatengeneza mzinga?

**Mama:** Mwanangu huo ni msemo tu, una maana kwamba unapofanya kitu kizuri utatamani kuongeza zaidi.

**John:** Kumbe ndivyo hivyo

**SWALI**

Kinyonga ana tabia gani kubwa ambayo anatumia kujilinda?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Unajua mambo yanayoua imani ya watu walio wengi?

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada yetu kuhusu imani. Wiki iliyopita nilijadili swali kwamba mbona watu wengi wasipoona kwa macho ya mwili hawaamini? Niliahidi kutaja mambo yanayoua imani ya watu wengi.***

Lakini kabla sijaendelea, hebu sikia ushuhuda huu kuinua imani yako. Kijana mmoja mwanafunzi huko Marekani, alipewa kazi ya kuwahi shuleni kila siku asubuhi ili kuwasha moto jiko litoalo joto vyumba vya madarasa kwani ilikuwa majira ya baridi kali.

Siku moja walimu na wanafunzi walipofika shuleni, wakakuta shule inawaka moto na yule kijana ameungua vibaya na kupoteza fahamu. Wakamkimbiza hospitali na mama yake kuambiwa na madaktari kuwa hakuna uwezekano wa kijana wake kupona.

Kwa mbali akiwa katika maumivu makali, kijana akasikia maelezo ya daktari kwa mama yake. Moyoni akaamua kwamba hata iweje hatakufa! Kwa mshangao wa madaktari, siku walizotarajia yule kijana kufa zikapita akiwa bado hai!

Hata hivyo, madaktari wakamwambia mama yake ingawa ameweza kupona hataweza kutembea maisha yake yote kwani ameungua vibaya kuanzia kiunoni hadi miguuni. Kijana akasikia tena maelezo yale akaamua kuwa atatembea kwa lazima. Hii tunaita 'imani kichaa'.

Kijana alipotolewa hospitalini akawa nyumbani akaanza mazoezi akiwa kwenye kiti cha magurudumu. Aliendelea kufanya mazoezi akitambaa chini, kujisimamisha kwenye uzio na hatimaye kutembea kwa shida!

Aliweza kupata nguvu taratibu, akaanza kutembea kwenda shuleni, mwishowe akawa anakimbia. Alifanikiwa kujiunga na timu ya riadha ya shule katika mashindano ya kitaifa, akavunja rekodi ya dunia ya maili moja iliyodumu kwa miaka mingi. Huyu ni yule aliyeambiwa na madaktari kuwa atakufa au kuwa mlemavu maisha yake yote. Jina lake, Glenn Cunningham.

Mungu aliyemuinua Glenn atakuinua na wewe msomaji wangu, kwa sababu alikuleta hapa duniani kwa kusudi maalum, na ni yeye pekee atakaye kuwezesha kufanikiwa. Unachopaswa kuzingatia ni kwamba Mungu anaweza yote, wewe ni kuamini tu usimtilie mashaka kwani yeye siyo mwanadamu aseme uongo, wala siyo mtu ajute!

Sasa nijielekeze kwenye mambo yanayoua imani ya wengi. Nilikuambia kuwa 'imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana'! Moja ya sumu kali zinazoua imani yetu ni kule kuzoea hali ya kushindwa. Tumeruhusu kushindwa kutujengea tabia hasi kiasi hata ukipata uhakika toka kwa Mungu bado unatilia mashaka!

Katika nchi ya utumwa, wana wa Israel waliruhusu hali ya kushindwa kuwaondolea tumaini lao kwa Mungu, hawakuwa tena na moyo wa kumsifu Mungu. Wakasema; Kando ya mito ya Babeli ndiko tulikoketi, tukalia tulipokumbuka Sayuni.

"Katika miti iliyo katikati yake, tulivitundika vinubi vyetu. Maana huko waliotuchukua mateka, Walitaka tuwaimbie, Na walituonea walitaka furaha; tuimbieni baadhi ya nyimbo za Sayuni. Tuuimbeje wimbo wa Bwana katika nchi ya ugeni?

Msomaji wangu, watu wanaoongea lugha hizi imani yao imekwisha kufa. Ikatae roho inayokufanya uzoee kushindwa. Jifunze katika kushindwa lakini usizoee kushindwa!

Wapo watu ambao hawatafanya jambo lolote wakihofia kushindwa, ni wepesi kuwadharau na kuwashutumu wale waliojaribu na kushindwa. Zitumie shutuma na dharau zao kama ngazi kuyapandisha mafanikio yako!

> **Katika miti iliyo katikati yake, tulivitundika vinubi vyetu. Maana huko waliotuchukua mateka, Walitaka tuwaimbie, Na walituonea walitaka furaha; tuimbieni baadhi ya nyimbo za Sayuni.**

Mpenzi msomaji, bila shaka unaendelea kufunguliwa ufahamu wako kuhusu nguvu ya imani na jinsi inavyopaswa kufanya kazi ndani yako. Nimalizie kipengele hiki kwa ushuhuda ufuatao;-

Mtu mmoja alikuwa na Punda ambaye aliamua kumuua kwa sababu aliona hana faida kwake. Akachimba shimo refu akamtumbukiza huko akiwa hai. Akawa anamrushia udongo kumfukia. Kila alipomwaga udongo, punda alilia sana akijua mwisho wake umefika.

Katika ile hofu ya kufa, yule punda akili ikafunguka kila udongo uliporushwa alijitikisa na kupanda juu yake. Alifanya hivyo kila aliporushiwa udongo, hatimaye akajikuta amefika juu ya shimo akatoka na kukimbia.

Unaweza kuruhusu lawama na shutuma kukufunika na kuua imani yako au unaweza kuzitumia kama ngazi ya kuinua imani yako . Kumbuka; Mbwa aliyekufa hapigwi mawe!

***Wiki ijayo nitaendelea na maeneo mengine yanayoua imani yake. Je, una maoni, kisa cha kimaisha ungependa tujadili pamoja? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Tutumie Royal Tour kujitangaza, kujiimarisha kiuchumi

FILAMU ya Royal Tour iliyochezwa na Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa kama mwongoza watalii akimwongoza Mwandishi Peter Greenberg, ambaye alitembezwa na kuelezwa kwa kina kuhusu vivutio vilivyopo nchini vitakavyomfanya mtu yeyote atamani kutumia fedha na kukaa zaidi nchini kwetu ina manufaa makubwa.

Katika filamu hiyo, Rais Samia anaonekana kumudu vyema kazi yake ya kuongoza watalii kwa kumweleza kuhusu vivutio kwenye Hifadhi za Taifa na Zanzibar.

Pia Rais alionekana akimwendesha mgeni wake kwenye gari la watalii huku akimweleza na mtalii akiuliza maswali mengi ya kutaka kujifunza zaidi au kufurahia safari yake anapokuwapo nchini.

Ukitazama sehemu ndogo ya filamu hiyo iliyoachiwa kwenye mitandao, utaona namna gani inatengeneza hamu au sababu ya mgeni kutoka taifa lolote anapopanga safari yake kufikiria pa kwenda ni Tanzania pekee na si kwingine.

Mara nyingi tumeona jitihada za nchi jirani kujitangaza kwa kutumia vivutio vilivyoko nchini kwao hata vile vilivyoko mpakani, wanavitumia ili kuwavutia watalii.

Mathalani, niliwahi kwenda Geneva, Uswisi nikaona mabasi na treni kwa wiki moja ambayo kulikuwa na mkutano wa dunia wa masuala ya majanga, yakiwa yamepambwa picha za Mlima Kilimanjaro, hifadhi za taifa na wanyama watano wakubwa wanaopatikana nchini lengo likiwa ni kutengeneza sababu kwa nini mtalii atembelee kwao.

Nilipofika uwanja wa ndege, niliona kwenye mbao za matangaza za ndani na nje wameweka Mlima Kilimanjaro na wanyama hao kuendelea kumshawishi mtalii kupanga safari na kuifanya ya nchi hiyo kuwa kituo chake muhimu.

Ndani ya ndege ya Shirika la Ndege la Uturuki, nilikuta jarida ambalo ndani yake kulikuwa na makala iliyoandikwa kwa ustadi ikiambatanishwa na picha mbalimbali, kuendelea kutengeneza sababu ya mtalii kwenda nchini humo.

Kama Mtanzania, nilisikitika kwa nini sikuona makala ya nchi yangu wakati naelewa fika Mlima Kilimanjaro uko nchini kwangu, ukitaka kuupanda vizuri kwa njia nzuri na kuuona vizuri lazima upandie Tanzania lakini ukitaka kuona nyumbu wanavyohama lazima uje upande wa Tanzania.

Kama haitoshi nyumbu wote wana hati za kusafiria za Tanzania kwa kuwa lazima wakabebe mimba Masai Mara waanze kurudi taratibu wakipita kituo hadi kituo ikiwamo eneo la mtawanyiko la Loliondo, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCA) na baadaye kurudi Hifadhi ya Taifa Serengeti ambako huzaliana na ikiwa kutakuwa hakuna mvua basi wana uwezo wa kuahirisha kuzaa hata kwa miezi mitatu.

Filamu hii ni muhimu mno kwa taifa, kwa sekta binafsi na serikali ikiwa wataziona fursa zilizoibuliwa, mathalani Mtanzania wa kawaida kabisa anaweza kujiuliza hiyo filamu inamsaidia nini na kwa jinsi gani itaboresha maisha yake.

Watalii wanapoongezeka kwenye hifadhi na vivutio vyetu ndiyo mapato, ajira za kudumu na huduma za kijamii zinaongezeka. Mwekezaji atajenga hoteli atahitaji watu wa kuajiri, atanunua bidhaa kutoka kwa wakulima, wananchi watauza bidhaa za utalii au zinazoendana na utalii kama vitu vya utamaduni, vyakula vya asili na kuonyesha utamaduni kisha watapata kipato.

Pia kuna maeneo yaliyohifadhiwa na jamii yanayojulikana kama Wildlife Management Areas (WMA) ambayo wanyama hupita kwenda hifadhi nyingine, wanajipatia kipato kwa kuwa na wawekezaji. Mathalani, Burunge WMA waliwahi kupata Sh. bilioni 2.2 ambazo Sh. bilioni 1.1 ilikwenda serikalini na iliyobaki iligawanywa kwenye vijiji ambavyo vilipata wastani wa Sh. milioni 100.

Kupitia utalii wamefanya miradi mingi ya huduma za kijamii na ni moja ya vijiji vyenye ofisi nzuri ambazo zinaweza kufanana na za baadhi ya halmashauri nchini.

Katika kila hifadhi, kuna ujirani mwema, kwamba sehemu ya mapato yanarudi kwa jamii kupitia vipaunbele vyao vya huduma za kijamii kama elimu, afya, na miundombinu ya maji na barabara ambavyo ni kwa faida yao.

Kwa ujumla, kwenye utalii kuna ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja, hivyo filamu hii itakapoanza kuleta matokeo ni lazima tuyatumie vizuri kwa manufaa yetu binafsi, maeneo yetu na taifa kwa ujumla.

Lazima kila mmoja katika eneo lake ikiwamo sekta binafsi kujiandaa kunyonya fursa zilizopo, ili kuona umuhimu wa kazi kubwa iliyofanywa na Rais Samia ya kuongoza watalii kwa lengo la kuitangaza Tanzania duniani na kutengeneza sababu ya kwanini mtalii achague kutumia muda na fedha zake hapa nchini na siyo kwenda kwingine.

Katika mahojiano ya Rais Samia na Mwandishi Peter, alisema moja ya mambo ambayo mgeni yeyote hatajutia kwa kuja nchini, ni ukarimu wa Watanzania, jambo ambalo ni kweli limekuwa utanaduni wetu kukirimu wageni kwa mengi na tunasifika Afrika kwa ukarimu mkubwa.

# HARUSI





Mwezi mtukufu wa Ramadhan ni kipindi cha kuonyesha mambo mema, katika picha ni baadhi ya mavazi yanayofaa kuvaliwa wakati wa kufunga ndoa katika kipindi hiki cha mfungo.





# MITINDO

## MAPAMBO YA VITO





# Huendana na vazi maalumu

MITINDO ya mavazi ya kisasa yanakwenda sambamba na aina mbalimbali ya mapambo ambayo yatamfanya mtu kuwa na mwonekano wa kipekee.

Kutokana na mvuto wa kipekee unaoletwa na mapambo ndani ya vazi, kumekuwa na ongezeko la watu ambao wanapenda kuyatumia kama njia ya kuwaongezea mvuto.

Wataalamu wa masuala ya mitindo wanasema matumizi makubwa ya mapambo kama yale ya kiasini au vito vya madini ni muhimu kuangalia aina ya nguo, eneo au muda husika.

Wanasema baadhi wanachanganya matumizi na wakati mwingine wanatumia kwa kuiga wenzao.

**JINSI YA KUCHAGUA**

Mapambo yanayotokana na madini ya dahabu, shaba na fedha kama pete, hereni, vipini, mikufu na mikanda ya kiunoni yanaendana na mavazi yenye heshima na kisasa zaidi.

Unatakiwa kuhakikisha mapambo ya aina hii kutochanganya na aina nyingine ya vito.

Ukitumia mapambo yenye madini ya Almasi na Rubi unatakiwa kuambatana na vazi lenye mitindo ya kisasa lakini liwe maalum kwa sababu mara nyingi inamfanya mtu aonekane mwenye uwezo mkubwa wa kifedha.

Unashauriwa kuhakikisha hakuna kitu kingine cha madini kipo karibu na pambo lako.

UREMBO



KOPE ZA ASILI

# Tumia njia hizi utapenda

IMEKUA tabia ya wanawake wengi kuweka kope za bandia bila kujali aina ya madhara yanayoweza kutokana na matumizi hayo.

Leo tunawaletea njia rahisi ya kukuza nyusi au kope zako kwa njia ya asili ukiwa nyumbani kwako.

Huna haja ya kwenda saluni kuweka kope kwa gharama kubwa na kuhatarisha usalama wako.

Vitu vinavyotumika unaweza kuvinunua ukawa navyo nyumbani kwako hasa brashi la kupakia mascara.

Faida ya kutumia njia hii kukuza nyusi au kope zako, zinakua zako moja kwa moja kwa hiyo muonekano huu ni wa milele.

**HATUA ZA KUFANYA**

Safisha vizuri brashi yako ya mascara ili kuondoa ule weusi wa mascara.


Ukishasafisha hakikisha unaikausha kwa kitambaa au taulo safi kabla ya kuanza kutumia.

Kama ulikua umepaka 'make-up' au umepaka mafuta yoyote nawa ili uso wako uwe mkavu.

Chukua brashi yako na uiweke mafuta ya vaseline na uanze kupaka kwenye nyusi zako au kope.

Fanya hivi kwa muda wa wiki na utaona matokeo unaweza kuendele kufanya mpaka pale utakapo ridhishwa na urefu wa nyusi au kope zako.

Hakikisha unapaka mafuta hayo kwenye kope zako wakati wa usiku.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Mayai chakula cha haraka

MAYAI ni chakula chepesi na chanzo kikubwa cha Protini. Unaweza kula chakula hiki muda wowote maana ni rahisi kuandaa na pia kitamu.

**MAHITAJI**

Mayai manne, vitunguu viwili, karoti mbili, pilipili hoho moja, kitunguu saumu punje mbili, pilipili manga kijiko kimoja kidogo na chumvi.

**NAMNA YA KUANDAA**

Andaa kitunguu maji na kitunguu saumu, menya kisha kata vipande vidogo.

Osha kisha kata pilipili hoho vipande vya wastani. Menya kisha kata karoti kwenye vipande vidogo na hifadhi pembeni.

Pasua yai, weka chumvi kama unavyopenda, koroga vizuri na hifadhi pembeni.

**NAMNA YA KUPIKA**

Bandika kikaango jikoni acha kipate moto, kisha weka mafuta ya kula. Yakipata moto, weka kitunguu saumu, kitunguu maji.

Koroga vizuri hadi viive. Koroga pamoja, funika acha viive. Baada ya dakika mbili hadi tatu, weka pilipili hoho na karoti kisha koroga pamoja. Acha viive kwa dakika tatu.



Mwagia yai kwenye kikaango, koroga vizuri ili lichanganyike na mboga za majani. Acha liive vizuri upande mmoja, kisha geuza.

Unaweza kuvuruga ili kupata vipande vidogo vidogo au unaweza kuacha liungane kama chapati.

Unaweza kula yai hili kwa chakula chochote kile, ugali, wali, au kama kitafunwa chepesi wakati wowote.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



## Fahamu tofauti Home Theatre, Subwoofer



KAMA sio mpenzi wa mziki wa sauti ya juu ni vigumu kutambua redio kubwa unayotumia kama ni Subwoofer au ni Home Theatre.

Je kuna tofauti na hivi vitu viwili? Na kitu gani imara na unaweza kukitumia ukiwa na furaha ndani ya nyumba yako?

Majibu sahihi ambayo nayo inatokana na maelezo ya watu mbalimbali ni kama ifuatavyo.

**1:** Home Theatre huu ni mjumuisho wa vifaa vya sauti na picha ambapo kwa pamoja hutengeneza mazingira ya sauti kama tunazo zisikia kwenye majumba ya sinema ndio maana Home Theater pia hufahamika kama 'Home Cinema' yaani sinema majumbani.

**2:** Sub Woofer ni kifaa kinachojitegemea ni spika ya besi ambayo ina njia ya kugawa sauti katika spika zingine za ziada.

**3:** Subwoofer haina spika nyingi kama Home Theatre ambayo inajitegemea kwa kuwa na vifaa vingi ikiwamo chombo cha kuchezesha DVD, CD na kanda.

**4:** Home Thetre sauti yake haina kero masikioni kama ilivyo Subwoofer ambayo midundo yake inakuwa mizito na wakati mwingine inaleta usumbufu.

# Tambua athari za kujenga katika udongo wa mfinyanzi

KUNA mambo mengi ambayo huchangia kuleta athari kwenye nyumba na hili tumekuwa tukijifunza kutoka katika maelezo ya watalaam mbalimbali kwenye sekta hiyo.

Watalaam hao wamekuwa wakisema kama ilivyo kwa vitu vingine kukumbana na changamoto mbalimbali, pia uchaguzi wa eneo la ujenzi wa nyumba linahitaji umakini mkubwa.

Miongoni mwa vitu ambavyo vimekuwa vikisisitizwa na wataalam hao ni pamoja na suala la kuzingatia au kuepuka kununua kiwanja na kujenga nyumba katika eneo ambalo linaweza kusababisha athari kwenye nyumba yako baadaye.

Baadhi wamekuwa wakishauri kwamba japokuwa si utaratibu wa watu wengi, ni vyema na kwa usalama wa nyumba, kujenga utaratibu kabla ya kununua kiwanja kwa ajili ya matumizi ya ujenzi wa nyumba, ukawaona wataalam wakakushauri kama ni salama au la.

Katika safu hii leo, mtaalam wa shughuli za ujenzi, James Mushi, anaeleza athari za kujenga nyumba kwenye kiwanja chenye udongo wa mfinyanzi.

Anaeleza kwamba udongo wa mfinyanzi una tabia ya kuvimba na kuongezeka ukubwa hasa unapopata maji na pia unapokauka husinyaa.

"Kwa maana hiyo, udongo unapovimba na kuongezeka ukubwa, jengo hunyanyuliwa juu, lakini udongo unaposinyaa jengo hutitia,"anaelezea mtaalam huyo.





"Kuna aina nyingi za udongo wa mfinyanzi na katika kila aina ya udongo huo hutofautiana na aina nyingine katika kuvimba au kusinyaa na hii inasababishwa na kiasi cha unyevunyevu kwenye ardhi husika," anasema Mushi.


Anasema udongo huo wa mfinyanzi huvimba zaidi wakati miti iliyomo kwenye eneo husika linalotumika kujenga nyumba inapokatwa.

"Udongo hasa wa mfinyanzi huvimba zaidi wakati miti iliyomo inapokatwa, na hii inatokea kwa sababu mizizi hukomaa zaidi na kunyonya maji kwenye ardhi na kuchangia ongezeko la kiasi fulani cha unyevunyevu kwenye udongo huo,"anasema Mushi.

"Na kuondolewa kwa maji kwenye udongo wa aina hiyo ya mfinyanzi kwa kunyonywa na mizizi ya miti husababisha udongo kuongezeka au kupungua ujazo kwa kiasi fulani husasani katika kipindi cha kiangazi au masika," anasisitiza.

"Na kuvimba au kusinyaa huko kwa udongo ni hatari kwa msingi wa nyumba kwa sababu huchangia kuleta nyufa kwenye nyumba na wakati mwingine kuiharibu kabisa.," anashauri.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
WE'BABA POLEPOLE! TUHESHIMIANE KICHWA CHANGU SIO NGOMA UJUE!
UMEKUJA MWENYEWE SIJAKUITA
NENDA UENDAKO LAKINI UKIONA "TUMEFUNGWA" USIRUDI NIMEJI-PANGA SITAKI KERO!
UKIONA KIFARU UJUE NI MIMI MPANGAJI WAKO NARUDI
KILA NIKISOMA BANGO LA SHELI KILA NILIONAPO PRESHA JUU!
TATIZO GANI?
NAOTEA MUMEO NDIO MME WAKO BISHA?
KHAAA!!! WE BABA UMEJUAJE?
MUME WANGU KANI-AHIDI TALAKA WAKI-FUNGWA HUKO SAUZI
MIE TUMEPINGA ATANIOA
MTANI DUA ZAKO NDIO NAKWENDA KUKINUKISHA NA 'OLANDO'
NAKUOMBEA UKAKOGE NYINGI
KULE 'FEI TOTO' HUKU 'MAYELE' PALE KUNA 'INONGA' PEMBENI 'KAGERE' NAKWAMBIA SAUZI OLANDO HATOKI!
VUA MAPEMA NGUO ZAO!
TUTAKULETEA PESA YAKO MECHI IKIMALIZIKA KWA SABABU UMESEMA TUTA-SHINDA LAZIMA
NA MKIFUNGWA JE?
UTAFURAHIA SHOO'
RANGI YA 'MISOFA' YA HUMU MJENGONI KWA SISI 'WANAINCHI' TUNAKALIA BASI TU!
PRESHA YA MECHI YA LEO BORA NIKAFIE KWETU KULIKO KUSAFI-RISHWA MAITI
SANDA UME-NUNUA?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
,,,MACHOZI HAYALETI FURAHA...FURAHA HULETA MACHOZI...

# Uingereza yatilia shaka ushindi wa Russia

## ■Majasusi wasema hakuna hatua mpya

LICHA ya kuongezeka kwa shughuli mbalimbali, vikosi vya jeshi la Russia havijafanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Tathimini hiyo imetolewa na Idara ya Ujasusi ya Ulinzi (DI) ya wizara ya ulinzi ya Uingereza, ikieleza hali hiyo inatokana na vikwazo vilivyowekwa na wanajeshi wa Ukraine.

Taarifa hiyo ilisema vikosi vya anga na majini vya Russia havijaweka udhibiti katika eneo lolote kutokana na jitihada za ulinzi wa anga na bahari wa Ukraine kupunguza uwezo wao wa kufanya mashambulizi makubwa.

Pamoja na ushindi uliotajwa wa Mariupol, kusini-mashariki mwa Ukraine, bado mapigano makali yanaendelea na kukatisha tamaa majaribio ya Warussia kuudhibiti mji huo.

"Hii inapunguza kasi ya jitihada za Russia katika eneo la Donbas mashariki mwa Ukraine," ilisema DI.

Mapema wiki hii, Russia ilitangaza hatua ya pili ya operesheni yake maalum ya kijeshi nchini Ukraine, ikisema sasa itazingatia kuchukua udhibiti wa Donbas.

Haya yanajiri baada ya wanajeshi wa Russia kujiondoa kutoka kaskazini-mashariki mwa Ukraine, baada ya kushindwa kuchukua miji mikubwa ikiwa ni pamoja na mji mkuu wa Kyiv.

Russia ina malengo ya kuchukua udhibiti kamili wa kusini mwa Ukraine na pia eneo la mashariki la Donbas, kama kamanda mkuu wa alivyosema.

Meja Jenerali Rustam Minnekayev, alinukuliwa katika vyombo vya habari vya serikali akisema lengo hilo lingeruhusu kuunda daraja la ardhini kuelekea Crimea, ambalo ililinyakua mnamo 2014.

Pia alisema itaipa nchi yake ufikiaji wa eneo la kujitenga linaloungwa mkono la Transnistria huko Moldova.

Transnistria ni eneo dogo linalopakana na magharibi mwa Ukraine.

Haijawekwa wazi kama maoni ya Jenerali Minnekayev yaliidhinishwa rasmi na Ikulu ya Kremlin, lakini yalinukuliwa sana katika vyombo vya habari vya serikali ya Russia ikiwa ni pamoja na mashirika ya habari ya Interfax na Tass.

Maofisa wa ulinzi wa Russia walimwambia mwandishi wa BBC Steve Rosenberg kwamba wanachunguza" maoni ya jenerali huyo, ambayo ikiwa yatathibitishwa yanatoa ufahamu wa kwanza kuhusu mipango inayoweza kutekelezwa na nchi hiyo katika wiki zijazo.



Moshi ukifuka kutoka kiwanda cha chuma cha Azavtal baada ya kushambuliwa na wanajeshi wa Russia katika mji wa bandari ya kusini wa Mariupol, Ukraine juzi. **PICHA: DW**

### MARIUPOL WAGUNDUA KABURI LA PILI LA HALAIKI

Meya wa mji wa Mariupol nchini Ukraine, amesema wamegundua kaburi lingine la halaiki nje ya mji huo. Halmashauri ya mji ilichapisha picha ya satelaini iliyotolewa na shirika la Planet Labs, ikionesha kile ilichosema ni kaburi la watu wengi lenye ukubwa wa mita 45 kwa 25, ambalo linaweza kuwa na maiti za raia wasiopungua 1,000 wa Mariupol.

Alisema kaburi hilo la halaiki liko nje ya kijiji cha Vynohradne, mashariki mwa Mariupol.

Mapema wiki hii, picha za satelaiti kutoka kampuni ya Maxer Technologies zilifichua kile kilichoonekana kuwa makaburi mapya zaidi ya 200 yaliyochimbwa katika mji wa Manhush, uliopo magharibi mwa Mariupol.

Ugunduzi wa makaburi hayo ya halaiki ulisababisha shutuma kwamba Warussia wanajaribu kuficha mauaji ya raia mjini humo

### MAREKANI KUITISHA MAZUNGUMZO

Makao makuu ya jeshi la Marekani Pentagon, yamesema Waziri wa Ulinzi Lloyd Austin, ataitisha mkutano wiki ijayo nchini Ujerumani.

Viongozi watakaohudhuria ni maofisa wa ulinzi na wa kijeshi kutoka zaidi ya mataifa 20, ili kujadili mahitaji ya haraka na ya muda mrefu ya kiulinzi kwa Ukraine.

Msemaji wa Pentagon, Jorn Kirby, alisema kuwa karibu mataifa 40, yakiwemo wanachama wa jumuiya ya kujihami NATO, yamealikwa na kwamba majibu bado yanaendelea kuja kwa ajili ya kikao hicho kitakachofanyika kwenye kambi ya jeshi la anga ya Ramstein.

Mkutano huo unakuja wakati Russia ikijipanga kwa kile kinachotarajiwa kuwa mashambulizi makubwa mashariki mwa Ukraine.

Kirby alisema mkutano huo utajadili tathmini mpya ya mapambano ya Ukraine pamoja na juhudi za kuendeleza mtiririko wa silaha na msaada mwingine wa kijeshi.

Yatahusisha pia mahitaji ya kiulinzi ya Ukraine baada ya vita lakini alisema hakitarajiwi kuzingatia mabadiliko kuhusu msimamo wa kijeshi wa Marekani barani Ulaya.

### UHARIBIFU UMEFIKIA HASARA YA BILIONI 60

Uharibifu wa majengo na miundombinu ya Ukraine kutokana na uvamizi wa Russia umefikia hasara ya takriban dola bilioni 60 na utaongezeka zaidi kadri vita vinavyoendelea.

Rais wa Benki ya Dunia, David Malpass, alisema hayo wakati wa mkutano wa Benki hiyo kuhusu mahitaji ya msaada wa kifedha kwa Ukraine ambao makadirio ya awali ya gharama yalikuwa madogo kuliko gharama za kiuchumi zinazoongezeka.

> **"Haijawekwa wazi kama maoni ya Jenerali Minnekayev yaliidhinishwa rasmi na Ikulu ya Kremlin, lakini yalinukuliwa sana katika vyombo vya habari vya serikali ya Russia ikiwa ni pamoja na mashirika ya habari ya Interfax na Tass.**

Malpass alisema vita bado vinaendelea, kwa hivyo gharama zinaongezeka.

Rais wa Ukraine akihutubia kwa njia ya mtandao mkutano huo uliofanyika mjini Washington , alielezea gharama kubwa zaidi na mahitaji ya kifedha.

Aliwaambia washiriki katika matamshi yaliyotafsiriwa kuwa Ukraine inahitaji dola bilioni 7 kwa mwezi kufidia hasara ya kiuchumi iliyosababishwa na uvamizi wa Russia dhidi ya nchi yake.

"Tutahitaji mabilioni ya dola kuijenga upya nchi baadaye," Zelensky alisema.

Alisema jumuia ya kimataifa inatakiwa kuiondoa Russia mara moja kwenye taasisi za kifedha za kimataifa, ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia na Shirika la Kimataifa la Fedha(IMF) na nyinginezo, na kusema nchi zote lazima ziwe tayari mara moja kuvunja uhusiano wote na Russia.

Waziri mkuu wa Ukraine Denys Shmyhal, ambaye alihudhuria mkutano huo ana kwa ana, alisema pato la taifa la nchi yake linaweza kuporomoka kwa asilimia 30 hadi asilimia 50, na hasara ya moja kwa moja na isiyo ya moja kwa moja ni jumla ya dola milioni 560 kufikia sasa.

Kiwango hicho ni zaidi ya mara tatu ya ukubwa wa uchumi wa Ukraine, ambao ulikuwa sawa na dola bilioni 155.5 mwaka wa 2020, kulingana na takwimu za Benki ya Dunia.

## MAKALA

# MAWASILIANO NDANI YA VYOMBO USAFIRI WA UMMA



Na Magabilo Masambu - 0689157789

MAWASILIANO ni taaluma ambayo inasomewa katika ngazi tofauti kama zilivyo taaluma zingine. Lakini asili inatupa uhalali wa kufanya mawasiliano bila hata kwenda shuleni kusomea, hivyo wakati mwingine tuna kuwa tunadhani kwamba tunafahamu kuwasiliana vyema kwa sababu ya kusikilizana na kuelewana.

Katika mawasiliano kupitia mazungumzo yetu ya kila siku, tunapeana taarifa ambazo zaweza kuwa katika kupashana pekee, kuelimishana au kuburudishana. Ziko taarifa nzuri vilevile na pia twaweza kupeana taarifa mbaya kama za ugonjwa au vifo.

Katika mawasiliano, ni muhimu sana wakati wa mazungumzo kuchagua taarifa za kuzungumza au kupashana kulingana na wakati, eneo lakini pia wahusika kwa maana ya ama unaozungumza nao au wanaokusikiliza. Ni lazima kujiuliza je, unaozungumza nao na wale wanaokusikiliza ni wahusika wa jambo hilo? Kama ni wahusika umejiridhisha kwamba mambo mnayozungumza yanawahusu? Kama hayawahusu wanapendezwa kuyasikiliza mazungumzo yako au yenu?

Nayasema haya kwa sababu pengine huwa ni mimi tu au kuna wengine pia huwa wanakerwa na tabia hii. Unakuta mtu yuko kwenye daladala kapigiwa simu kuhusu mambo binafsi, wakati mwingine si habari ya haraka ambayo ingehitaji utatuzi wakati huohuo. Ni habari ambayo hata kama angeshuka kwenye daladala baada ya kufika safari yake angelizungumza lakini anakazana kuzungumza tena kwa sauti ya juu.

Hivi kwa nini usimwambie anayekupigia simu kwamba tuzungumze baadaye ili kuepusha adha kwa abiria wenzio? Maana habari unazozungumza haziwahusu na wala hawahitaji kuzisikia lakini ndiyo kwanza unakomaa hivi huwa ni umbea kwamba ukimaliza mazungumzo upate wa kukuuliza na uanze kuteka mjadala kwenye daladala au huwa tunakwama wapi?

Unakuta mtu kapigiwa simu na mpenzi wake, mambo wanayozungumza yanahusu uhusiano wao na wakati mwingine ni mazungumzo yanayoashiria ugomvi kwamba hawako sawa. Je, unapoyazungumza kwenye halaiki kiasi hicho unataka kujionyesha kwamba wewe huna matatizo, bali mwenza wako ndiye mwenye matatizo au ni ushamba? Kuna haja gani sisi abiria wengine hatujawatuma mpendane mnatuhusisha ugomvi wenu? Unataka tukuulize baada ya kukata simu, tukusaidie ushauri au shida ni nini? Kwa nini usimwarifu kwamba mahala nilipo si vyema tukazungumza?

Wengine wanaotumia simu kubwa hizi (smart phone) kuchati nalo ni tatizo kubwa. Hapa ndipo kuna ushamba wa hali ya juu. Unakuta watu mmebanana kwelikweli, lakini mtu naye kakomaa kuwasha simu yake yuko kwenye makundi ya 'whaatsaap' au aina nyingine ya mtandao mbaya zaidi kawasha mwanga mkali utafikiri anatafuta sindano.

Hivi unajua kuna watu wana matatizo ya macho? Maana kila mtu anacho kiasi cha mwanga anachotumia kwenye simu,. Umewasha 'bright' mpaka mwisho lakini unafanya watu pia waanze kusoma meseji zako kwani huwezi kusubiri ukifika sehemu ukiwa peke yako uchati kwa uhuru na umekuwa utamaduni nafikiri pia ni ushamba wa matumizi ya simu janja.

Siku hizi mtu akishaketi tu kwenye daladala au hata amesimama jambo la kwanza ni kutoa simu, baada ya muda mfupi utaona kila mtu ana simu mkononi ni mwendo wa kuchati utafikiri kuna mashindano ya marathoni ya kuchati. Nakubali kwamba ni haki ya kila mtu kufanya mawasiliano, wala simaanishi nahitaji kuwapangia utaratibu wa muda gani wa kufanya mawasiliano kwa sababu sijawanunulia hizo simu, lakini kiungwana tu kama taarifa si ya lazima sana si vyema kuchati kwenye halaiki kama hii na ni vyema kuchagua taarifa za kuwasiliana pia huku tukijua kwamba wapo wanaokerwa kusikiliza mazungumzo yasiyowahusu.

Kwenye vyombo vya usafiri panakuwa na watu tofauti. Unaweza kujikuta umetoa taarifa ambazo zitawasaidia wengine kuzitumia maana unaweza kudhani hakuna anayekufahamu kumbe kuna mtu amejibanza kiti cha nyuma anakusikiliza jinsi unavyomsema fulani. Baadaye anafikisha taarifa tayari umeshalikoroga.

Ukiachilia mazungumzo ya simu, kuna mazungumzo ya ana kwa ana yaani mmeingia wawili au watatu kwenye gari, mnaanzisha mazungumzo kana kwamba mko sebuleni kwenu. Mnaongea kama walevi mpaka mnagonga na tano, mnatawala daladala kana kwamba mmeikodi kumbe mnalipa Sh. 400 kama wenzenu.

Ni kweli kwamba Katiba imetupatia uhuru wa kuzungumza na asili inatupatia uhalali huo lakini tusisahau kwamba tunaweza kujikuta tumeingilia uhuru wa watu wengine ikiwa ni pamoja na kusababisha makwazo. Kuna mtu amepanda humo ana matatizo yake ama ya ugonjwa au ya kimaisha tu, haitaji kusikia kelele za namna hiyo pengine maskini anadaiwa huko anatafakari namna ya kufanya lakini ninyi makelele kwelikweli. Kufanya hivyo kuna uwezekano tunawafanya wengine washuke vituo ambavyo hawakupanga kushuka kuepuka makelele.

Mwisho ni muhimu tunapokuwa kwenye vyombo vya usafiri wa umma, tutambue kwamba hatuko peke yetu na hatujakodi gari bali tunalipa nauli kama wanavyolipa wengine. Kwahiyo ni muhimu kulinda haki yao ya kulipa nauli kwenye daladala au basi si mahala pa kufanya mazungumzo yasiyowahusu watu wengine labda iwe imelazimika sana hakuna namna kwamba ni lazima taarifa au kazi hiyo ifanyike wakati huo huo, vinginevyo subiri ushuke Mtanzania.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Gezaulole, nyimbo za kijamaa wakati wa ujamaa



Na Adam Fungamwango

TUMEONEWA kiasi cha kutosha.Tumenyonywa kiasi cha kutosha. Unyonge wetu ndio uliosababisha tuonewe, tunyonywe na kupuuzwa.Sasa tunataka Mapinduzi. Mapinduzi ya kuondoa unyonge, ili tusionewe tena na tusipuuzwe tena". Yalikuwa ni baadhi ya maneno ya Rais wa kwanza wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akitangaza Azimio la Arusha mwaka 1967.

Lilipitishwa kwenye mji wa Arusha (sasa jiji) mwishoni mwa Januari mwaka 1967 na kutangazwa rasmi, Dar es Salaam, Februari 5 mwaka huo huo.

Katika misingi yake ilikusudia kulinda Uhuru wa Taifa, lakini sio tu Tanzania, bali na mataifa ya jirani ambayo kwa wakati ule yalikuwa katika tawala za kikoloni, misingi yake ililala katika ukombozi wa Afrika na Taifa na kufanya kuwa watu wa taifa huru pasi kuingiliwa na mabepari.

Pili ilikuwa kurudisha mali zote zilizokuwa zinamilikiwa na mashirika binafsi kuwa mali za serikali, maarufu kama mali ya umma zitakazomilikiwa na wakulima na wafanyakazi.

Kwa kutambua umuhimu huo, serikali ilihimiza wanachi kufanya kazi kwa bidii na kuzuia wanyonyaji.

Hapo ndipo nchi ilipoanza kwa kutaifisha mali za mabepari ambazo walikuwa wamejilimbikizia, pia kuanza kuanzishwa makampuni na kujengwa viwanda mbalimbali.

Ndipo vilipokuja Viwanda, Mashirika na Makampuni mengi ambayo mbali na kufanya makubwa, lakini mengi yalimiliki timu za mpira wa miguu, netiboli, ndondi, mpira wa wavu, na hata bendi za muziki wa dansi, kwaya na taarabu.

Vile vile baadhi vilimiliki hata vikundi vya ngoma za utamaduni ambazo kwa wakati huo vyote vilibatizwa jina la 'Kibisa', kutokana na kundi moja bora kabisa la aina hiyo, lililokuwa likimilikiwa na Shirikika la Maendeleo Dar es Salaam (DDC). Kundi hilo liliitwa DDC Kibisa Ngoma Troupe. Ndipo kwa kufupisha tu mashabiki waliita Kibisa kila kikundi ya utamaduni hata kama kilimilikiwa na kampuni au shirika lingine.

DDC pia ilimiliki bendi ya muziki ya dansi maarufu hadi leo, DDC Mlimani Park Orchestra, ikiwa na mtindo wake wa Sikinde Ngoma ya Ukae.

Tukirudi kwenye mada halisi, ni kwamba baada ya maneno ya Mwalimu, utekelezaji ukafanyika kama nilivyoainisha kuutaifisha na kuunda Mashirikika na Makampuni mengine, lakini pia watu walihimizwa kufanya kazi kwa bidii, na kuundwa Vijiji vya Ujamaa.

Siyo mikoani, hata Dar es Salaam, ambapo bado ilikuwa haijapanuka sana na maeneo waliyokuwa wanaishi zaidi watu ni Ilala, Kinondoni, Manzese na Magomeni. Sehemu kubwa iliyobaki ilikuwa pori.

Watu walihimizwa kutoka mijini kwenda vijijini kulima, na maeneo yalikuwa yakitolewa bure na serikali.

Lakini baadhi ya watu walikuwa wabishi, hawakutaka kwenda. Walipiga chenga, na hata waliokamatwa kwa nguvu kupelekwa, walikaa muda mfupi na kurejea tena mjini. Nyerere alikuwa na maono ya mbali sana. Kwani leo hii hao hao waliokuwa waking'ang'ania kukaa Manzese na kukataa kwenda Kunduchi na kupewa ardhi ya bure wanajuta, kwani ardhi yake ina thamani kubwa kwa sasa. Walioonekana wajinga wakati huo kwa sasa wamejenga majumba maeneo hayo ghali, wameingia ubia na matajiri au kuuza viwanja na kujipatia pesa nyingi ambazo zimewafanya kujenga majumba ya kifahari kwa sasa maeneo mengine na kuendesha biashara zao. Kama siyo wao, basi watoto wao au wajukuu wamenufaika.

Wanamuziki wa Tanzania hawakukaa kimya, kwani baada ya Azimio la Arusha walitunga na kuimba nyimbo nyingi sana kuunga mkono na kuwahimiza wananchi kufanya kazi na hata kwenda kujiunga na Vijiji Vya Ujamaa. Upo wimbo maarufu wa Urafiki Jazz, iliyokuwa inamilikiwa na Kiwanda cha Kutengeneza Nguo cha Urafiki maeneo ya Ubungo, Dar, uitwao 'Gezaulole' unaozungumzia kwa ufasaha jinsi watu walivyohimizwa kutoka mjini Dar, na kwenda pembezoni mwa mji wakati huo ambapo kulikuwa mapori kwa ajili ya kuanzisha maisha kwa kilimo. Maneno yake ni haya.

"Baba na mama shangazi na mjomba, mji hautufai, twendeni Gezaulole. Biashara ya kahawa na maji ya barafu, sasa haitufai twendeni Kibugumo. Songasonga na Kimbiji, Tegeta na Mwanadilatu, hayo ndiyo hasa maono ya mwana wa mapinduzi.

Kitambulisho cha Gezaulole ni jembe na panga lako, hiyo ndiyo satifiketi, ya mtu mwenye busara.

Gezaulole mama, Gezaulole mama eee. Biashara ya njugu na korosho sasa haitufai eee. Twendeni Kibugumo na Mwanadilatu kwenye makao mapya. Gezaulole mama ee, Gezaulole mama twende."

Hebu pata picha hapo. Maeneo yote yaliyotajwa hapo ya Dar es Salaam wakati huo, kwa sasa siyo mapori tena, ni miji iliyojengeka na hata viwanja kupatikana ni ghali sana. Kuna watu walikataa, sasa wanajuta. Wenzao waliokubali walipata bure kabisa.

Ujamaa ulitamalaki, lakini kuna baadhi walikuwa wakiupiga vita, lakini Mwalimu Nyerere alikaa imara kuueleza. Kurugenzi Jazz Band ya Arusha, wakatoa wimbo unaitwa 'Ujamaa' wenye maneno yafuatayo.

"Matumaini yenu Waafrika ni siasa ya Ujamaa. Njama mbinu za hali ya juu kuangusha ujamaa. Ujamaa ni mzuri kwenye kuleta usawa. Tutaendelea hatutarudi nyuma. Tulikwishajua matatizo tutashinda. Mawazo sahau ujamaa utakufa. Fungeni vibwebwe tujenge ujamaa."

Nchi ilikuwa ya kijamaa kweli kweli.

NUTA Jazz Band, wana Msondo Ngoma, haikubaki nyuma, nayo ilitoa wimbo unaitwa 'Kijiji Cha Ujamaa'

"Ndugu zangu, mimi sina kazi, sasa nitapata tabu. Siku nyingi nimefanya bidii, ili niweze kupata kazi, kujitahidi ndiyo nimehirahidi kazi, ndiyo siipati. Sasa nitafanya nini mie, ooo, nakufa.

'Ndugu zangu wamenieleza niende katika kijiji cha ujamaa, nikajiunge na wenzangu, nipate mahitaji yangu, shida ziniondoke. Kwa sasa naondoka, nakwenda zangu, katika Kijiji cha Ujamaa, nimechoka sasa mwenzenu na mambo ya mjini."

# HADITHI

# Ajenda ya siri-27

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**


UMATI ulikuwa kimya. Wengine walibaki midomo wazi wasiamini kile kinachotoka kwenye kinywa cha Jaji huyo. Baadhi ya kinamama walianza kububujikwa machozi kimya kimya.

"Mtuhumiwa huyu huyu ambaye alihukumiwa kunyongwa. Leo kibao kinaonekana kugeuka. Ni ajabu na kweli." Mwahija ambaye alikuja mara ya kwanza kutoa ushahidi wa kumuuzia dawa. Alichokisikia hapo hakuamini masikio yake. Naye machozi yalianza kumbubujika kama bomba la mvua. Msichana ambaye mara kwa mara alikuwa anakuja kwenye duka na kumuuzia dawa. Msichana ambaye hata yeye alifahamu kuwa ndiye muuaji halisi.

"Vielelezo vilivyoletwa hapa vinaonyesha kuwa mke wa marehemu alifanya mauaji haya akishirikiana na mtu huyo, ambaye inaonyesha wana uhusiano wa kimapenzi. Na kilichoonekana kwenye kufuatilia ushahidi ni kwamba walikitaka kifo cha marehemu kitokee ili wapate uhuru wa kuwa wote. Mke wa marehemu arithi viwanda na mali za zote za marehemu, ikiwemo kuwa pamoja na mpenzi wake ambaye vielelezo vimemtaja kwa jina la Mtola. Kabla ya kutoa uamuzi, ni kwamba kesi ya mauaji hapa bado ipo. Ni kwamba marehemu Hafidh Chilambo ameuawa kwa kuwekewa sumu kwenye chakula. Ila kilichopo hapa mtuhumiwa aliyetuhumiwa na mauaji haya si yeye. Nadhani sasa hii itawapa fursa wahusika kuwasaka watuhimiwa halisi. Baada ya hapo tunatoa uamuzi. Mtuhumiwa anaachiwa huru. Kuanzia sasa upo huru." Alimaliza Jaji Msemwa.

Kilitokea kimya kama cha sekunde 20 hivi. Nadhani hakuna aliyeamini. Wapo walioona kama vile hawahajamsikia Jaji vizuri. Wengine walijihisi kama wako ndotoni.

Ghafla vikasikika vigelegele, vilivyoambatana na vilio. Kila binadamu ana mapokeo yake linapokuja suala la furaha au huzuni. Hili lilikuwa la furaha. Wapo waliofurahi kwa kupiga vigelegele na wapo waliolipokea kwa vilio. Kwenye eneo hilo la Mahakama ya Rufaa, vilio vilikuwa vya aina mbili. Kuna waliokuwa wakilia kwa furaha na wengine kwa huzuni na woga.




**"Vielelezo vilivyoletwa hapa vinaonyesha kuwa mke wa marehemu alifanya mauaji haya akishirikiana na mtu huyo, ambaye inaonyesha wana uhusiano wa kimapenzi. Na kilichoonekana kwenye kufuatilia ushahidi ni kwamba walikitaka kifo cha marehemu kitokee ili wapate uhuru wa kuwa wote.**

"Mwanangu mwanangu siamini, uko huru mwanangu Tina? Binadamu kweli wabaya, wamekusingizia umeua mtoto wa watu. Hujawahi kuua hata mende wewe, nakujua nakujua Tina, mimi nilijua tu, basi ningefanyeje..." Ni kilio cha furaha iliyochanganyikana na huzuni kutoka kwa Bi Mtupeni, mlezi wa mtuhumiwa.

Ni yeye ndiye aliyekuwa wa kwanza kwenda kumkumbatia binti huyo. "Mama, nimetoka mama niko huru, sijaua mimi walinisingizia..." Tina alikuwa akimng'ang'ania mama yake wa hiari.

"Najua mwanangu, ulikuja kwangu kwa mara ya kwanza kuomba kazi, nikakupa hukuwahi hata kuniibia shilingi moja, leo uue mtu mwanangu, najuta kukubali walipokuja kukuomba na kukuchukua mwanangu. Hebu Mwasi nipe khanga nimbebe mwanangu."

Tukio lililoendelea pale ambalo lilikuwa kivutio ni Bi. Mtupeni kuchukua khanga na binti yake Mwasi na kumbeba Tina, binti aliyekuja kwake miaka kadhaa iliyopita kuomba kazi za ndani, kabla hajaombwa na kuchukuliwa na watu waliotumwa na Hellen Kisa, mke wa marehemu Chilambo ambaye alihitaji dada wa kazi.

"Mizimu ya baba na mama yako imeitika mwanangu. Wamekufa mama yako nitabaki kuwa ni mimi." Ni kama Bi Mtupeni alikuwa anatambika.

"Kazi nzuri Tinga."

"Kazi nzuri na kubwa umeifanya wewe Eddy. Kupeleleza na kukusanya ushahidi wa hili lililotokea halikuwa jambo la kitoto.

Wewe ni tunu ya Taifa, kwa jinsi ilivyokuwa imejifunga hii kesi, tulikuwa tunampoteza msichana huyu mdogo, nguvu kazi ya taifa huyu. Ni wewe umemuokoa."

Yalikuwa ni mazungumzo ya pongezi kwa watu wawili, ambao wote waliifanya kazi hii kwa ustadi sana.

"Unajua mimi mwanzoni, nadhani na watu wengi tulijua binti ameua ila atakuwa ametumwa na kuahidiwa pesa au ametumiwa bila yeye kujua kwa hiyo nilichodhani kazi nitakayoipata ni kushawishi apunguziwe adhabu, au watafutwe watu wengine ambao walikuwa nyuma yake. He, kuja kusoma na kusikiliza vielelezo ulivyonipatia, mwenyewe nilishangaa," Tinga alimpasha mwenzake.

"Hata mimi wakati naanza hii shughuli nilijua hivyo. Wakati napiga hatua moja hadi nyingine ndipo nilipoanza kubadili mawazo yangu. Kumbe binti hajahusika kabisa." Eddy naye atoa mawazo yake ya awali kabla ya upelelezi.

Ghafla walizungukwa na watu mbalimbali ambao walikuwa wakiwapongeza kwa kazi kubwa waliyoifanya.

Ni watu wa Haki za Binadamu na wa mashirika mbalimbali yanayohusu wanawake, jinsia, na madada wa kazi ambao walikuwa wakiifuatilia kesi hiyo tangu mwanzo. Waandishi wa habari nao pia walifika.

Siku zote Eddy huwa hataki kupongezwa, sifa na vitu vingine vinavyofanana na hivyo, ikiwemo kujulikana. Ndivyo alivyo kiasili, na ukichanganya na kazi yake. Alijitoa kama kawaida yake, akamwambia Tinga apokee hizo pongezi azungumze na waandishi jinsi ilivyokuwa mwanzo hadi mwisho.

Hatua tano baadaye alijikuta akikumbatiwa ghafla. Alikuwa ni Tina. "Ahsante kaka ahsante kaka nashukuru kwa kuniokoa." Wakati Eddy akifikiri ni kwa nini amejua kuwa yeye ndiye aliyesababisha atoke, wakati hakuwa wakili na alionekana kama wasikizaji wengine wote waliokuwepo, akamuona Bi. Mtupeni na familia yake. Hapo ndipo alipojua ni kwa nini.

"Ahsante, pole sana msichana mzuri, leo kwanza nenda nyumbani kapumzike, baada ya siku mbili nitakuja huko tuangalie jinsi gani tunaweza kufanya ili urudi shule ukasome, sawa?" Alimuuliza Tina akiwa anamshikashika kichwa chake ambacho sasa kilikuwa na upara.

"Kweli kaka?"

"Ndiyo, nitakulipia mimi ada, utaniambia unataka kusomea nini. Nikija Tandale kila kitu kitakuwa sawa, unasikia? Nadhani ukisoma baadaye unaweza kuondokana na mambo kama haya. Unaweza ukawa na akili ya kuanzisha biashara zako mwenyewe, kufanya kazi, au kujiajiri."

"Ahsate sana kaka 'angu, nimeambiwa na mama kuwa wewe ndiye umenisaidia hadi nimechiwa."

"Usijali mdogo wangu.

"Baba sijui mimi niseme nini, yaani mimi sina la kusema hapa, uuwiii..." Eddy alipoona Bi. Mtupeni ni kama mtu aliyepagawa, alimfuata na kumkumbatia. Halafu akamnong'oneza.

"Mama hapa watu wengi watakutazama, ngoja niite taksi kwa njia ya mtandao, iwarudishe nyumbani, halafu mimi niache hizi siku mbili, nitakuja huko tufanye tafrija fupi."

Akasalimiana pia na mumewe, akapongezwa kwa kazi kubwa. Kifupi ni kwamba eneo la Mahakama ya Rufaa lilionekana kama kuna sherehe fulani kutokana na kuachiwa kwa Tina.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# RAIS SAMIA AMPA NENO BABA WA RIHANNA

NI jambo la kufurahisha na inaweza kuwavutia wasanii maarufu nchini Marekani kutembelea Tanzania, baada ya kukamilika uzinduzi wa filamu ya Tanzania Royal Tour' uliofanyika majuzi jijini Los Angeles.

Katika uzinduzi huo, Rais Samia Suluhu Hassan, alikutana na kusalimiana na Ronald Fenty, ambaye ni Baba wa Msanii Maarufu Rihanna.

Ronald alikuwa miongoni mwa watu waliokwenda kuangalia filamu hiyo katika ukumbi wa Paramount Pictures na kuonekana kuvutiwa na filamu hiyo.

# Jescalay Dasilver aibuka na DET

BAADA ya kimya cha muda mrefu mwimbaji wa Bongo Fleva, Brooklyn Mpemba, maarufu kama Jescalay Dasilver, ameibuka kivingine na wimbo mpya unaoitwa 'DET'.

Akizungumzia ujio wake mpya, Jescalay, ametamba kuwa alikaa kimya ili kujipanga na sasa anashukuru amekamilisha kila kitu hivyo muda wowote kutoka sasa wajiandae kupata burudani.

"Muziki wa sasa una changamoto nyingi na tunahitaji kujipanga ili kuwapata mashabiki wapya, nimerudi kivingine na ngoma yangu mpya ya DET ambayo itapatikana kwenye mitandao yote ya muziki duniani," amesema Jescalay.



## ZISIKUPITE

### JESUS ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL inangalia uwezekano wa kumleta straika wa Manchester City, Gabriel Jesus, 25, kwenye uwanja wa Emirates, huku Mkurugenzi wa ufundi wa washikabunduki hao, Edu akiwa amefanya majadiliana na wawakilishi wa rai huyo wa Brazil. ***(Athletic)***

### SALAH ATAKA KUBAKI

MOHAMED Salah, 29, anataka kubakia Liverpool lakini majaliwa ya mkataba wa muda mrefu bado hajajulikana, huku kukiwa hakujafiwa kwa makubaliano yoyote. ***(Four Four Two)***

### MBAPPE MKATABA MNONO

KLABU ya Paris St-Germain imempa ofa mshambuliaji wake, Kylian Mbappe, 23, mkataba huo una thamani ya euro milioni 50 kwa mwaka na utamfanya kuwa mchezaji anayelipwa zaidi klabuni hapo. ***(Goal)***

### CONTE AITAKA PSG

KOCHA wa Tottenham, Antonio Conte anataka kuinoa PSG msimu ujao na ana uhakika wa kuchukua mikoba ya kocha wa zamani wa Spurs, Mauricio Pochettino pale kwenye viiunga vya Parc des Princes. ***(Le Parisien)***

### NAVAS KUTUA NEWCASTLE

NEWCASTLE inajiandaa kumsajili golikipa wa PSG, Keylor Navas, 35, ambaye ataondoka hapo kwa vinara wa Ligue 1 kipindi cha majira ya joto. ***(Fichajes)***

### RICE OFA MPYA

DECLAN Rice, 23, amekataa ofa ya tatu ya mkataba kutoka West Ham ambayo itamfanya alipewa mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki. Kiungo huyo wa England anawaniwa na Manchester United na Chelsea. ***(The Guardian)***

### DUMFRIES AWANIWA SPURS

TOTTENHAM Hotspur imefanya mawasiliano na Inter Milan kuhusu usajili wa mlinzi wa kulia wa Uholanzi, Denzel Dumfries, 26. ***(Tuttosport, via Sport Witness)***

### VICKERS SAFI SPURS

KLABU ya Celtic ipo kwenye hatua nzuri ya mazungumzo na Tottenham Hotspur ili kumsajili mlinzi wa kati wa Marekani, Carter-Vickers, 24, kwa mkataba wa kudumu. ***(SBI Soccer)***

### RODON KUONDOKA

MLINZI mwingine wa Tottenham, Joe Rodon, 24, ameambiwa anaweza kuondoka klabuni hapo. ***(Football Insider)***

### BENOIT, DIABY SOKONI

NEWCSTLE inamwania mlinzi wa Monaco, Benoit Badiashile, 21, na winga wa Bayer Leverkusen, Moussa Diaby, 22. ***(Foot Mercato)***

### RUDIGER HAENDI KOKOTE

MLINZI wa Chelsea, Antonio Rudiger, 29, ameondoa uwezekano wa kuhamia Manchester United. Raia huyo wa Ujerumani atakuwa mchezaji huru mwishoni msimu huu. ***(Ben Jacobs, CBS)***

## DONDOO ZA SO
## MAGAZETI YA UL



# RALF AFUNGUKA HATIMA YA POGBA

### ●●● Asema kiungo huyo Mfaransa hawezi kubakia Old Trafford kutokana na...

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa muda wa Manchester United, Ralf Rangnick amesema, Paul Pogba "ana uwezekano mkubwa hatabaki" katika klabu hiyo zaidi ya msimu huu.

**Pogba alipata jeraha la mguu katika kichapo cha 4-0 kutoka kwa Liverpool Jumanne ambacho kitamweka nje kiungo huyo kwa mwezi mmoja.**

Huku Mfaransa huyo akimaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu huu, na mchezo wa mwisho wa United wa 2021-22 utapigwa Mei 22, mwaka huu, Rangnick hatarajii kuona Pogba atashiriki tena, na sasa amesema anaweza kuwa ameichezea klabu hiyo mechi yake ya mwisho.

"Hatapatikana (dhidi ya Arsenal) (jana) na kuna uwezekano mkubwa hatakuwapo kwa mechi zilizobakia. Inaonekana kwa sasa hataongeza mkataba wake (kwa hiyo) kuna uwezekano mkubwa hatakuwa hapa tena msimu ujao," alisema Rangnick katika mkutano na wanahabari Ijumaa kuelekea mchezo wa jana Jumamosi dhidi ya Arsenal.

Pogba amekuwa akihusishwa na kuhamia Real Madrid, Paris Saint-Germain na klabu ya zamani ya Juventus wiki za hivi karibuni.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 alishinda Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa mwaka 2018, akicheza nafasi ya nyota katika timu hiyo ya Les Bleus, lakini amekuwa na shida kucheza kwa kiwango cha juu mara kwa mara kwa United tangu arejee katika kilabu hiyo ya Ligi Kuu England mwaka 2016.

Alipoulizwa kwa nini miaka sita ya Pogba Old Trafford imekuwa ya kupanda na kushuka, Rangnick alijibu: "Ni vigumu kusema.

"Ni mchezaji aliyeshinda Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa, ni mchezaji mzuri kiasi alikuwa kawaida kuanza kwa timu kama vile Ufaransa. Sote tunajua ana uwezo wa aina gani na anaweza kuwa mchezaji wa aina gani.

"Alikuwa kama wachezaji wengine wachache wanaotatizika kupata utendaji wake bora uwanjani kwa timu kama United.

"Hili halijakuwa tu msimu huu au katika wiki kadhaa zilizopita. Ninavyokumbuka, ndivyo ilivyokuwa katika miaka ya awali."

SportPesa LIVE IN PLAY

MECHI KALI
LIVERPOOL
VERSUS
EVERTON
1 | 1.17
X | 6.70
2 | 12.81

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# POCHETTINO ANATAMANI MBAPPE KUBAKI PSG



**PARIS,** Ufaransa

MAURICIO Pochettino amesema angependa kumchukua, Kylian Mbappe "likizo" nyumbani kwake kama atamhakikishia anabaki Paris Saint-Germain.

Mbappe amebakiza zaidi ya miezi miwili katika mkataba wake wa sasa na PSG na mustakabali wake bado haueleweki.

Real Madrid wanaripotiwa na uhakika wa kumsajili fowadi huyo wa Ufaransa kama mchezaji huru, huku Erling Haaland akidhaniwa yuko njiani kuelekea Manchester City badala ya mji mkuu wa Hispania.

Pochettino anataka Mbappe asaini mkataba wa muda mrefu na PSG na anatumaini makubaliano yanaweza kufikiwa baada ya timu yake kutwaa tena taji la Ligue 1, jambo ambalo wanaweza kufikia iwapo jana Jumamosi wangevuna pointi moja dhidi ya Lens.

Aliwaambia waandishi wa habari: "Kama kocha, hali hiyo hainisumbui, lazima uelewe, hii haifanyiki Paris pekee, bali hata katika klabu nyingine.

"Hii si mara ya kwanza, wala si mara ya mwisho kwa hali kama hizi kutokea. Tunapaswa kuzoea. Kwa ubinafsi, ningependa kukaa naKylian, bila shaka.

"Ningependa kumchukua likizo, kumpeleka nyumbani. Klabu ingependa aweze kukaa hapa kwa muda mrefu. Ni mazungumzo.

"Uamuzi huu siku zote unahusiana na pande tofauti. Huenda ukachukuliwa mara tu lengo la taji litakapofikiwa, mara tu msimu unapomalizika."



## Guardiola: Kila mechi ni mtoano

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER, England
PEP Guardiola amesema Manchester City wanachukulia kila mechi kama ya mtoano katika harakati zao za kutafuta kutwaa taji la Ligi Kuu England na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

City wanaongoza kwa tofauti ya pointi moja dhidi ya Liverpool kileleni mwa msimamo wa Ligi zikiwa zimebakia mechi sita kabla ya kumenyana ya jana Jumamosi dhidi ya Watford kwenye Uwanja wa Etihad.

Pia watakuwa na faida ya nyumbani kwa mechi ya nusu fainali ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya vinara wa LaLiga Real Madrid, Jumanne ijayo.

Matumaini ya City kushinda mataji matatu yalihitimishwa walipofungwa 3-2 na Liverpool katika nusu fainali ya Kombe la FA kwenye Uwanja wa Wembley wikendi iliyopita, lakini wana nafasi kwenye Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Guardiola anajua hawawezi kumudu kuteleza katika kusaka mataji zaidi.

Alipoulizwa kama wanafikiri kwamba kila mchezo ni mtoano, bosi huyo wa City aliwaambia waandishi wa habari Ijumaa: "Hakika. Hatuwezi kuangusha pointi, lakini wao (Liverpool) pia hawawezi.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# BIASHARA UNITED KAMILI KUIDUWAZA MBEYA CITY

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Biashara United, Vivier Bahati amesema anaendelea kuusoma ubora wa Mbeya City kwa ajili ya kuhakikisha timu yake inapata ushindi watakapokutana katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Biashara United kutoka Musoma itafunga safari kuelekea Mbeya kuwakabili wenyeji Mbeya City katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Aprili 28, mwaka kwenye Uwanja wa Sokoine jijini humo.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Vivier alisema mechi za mzunguko wa pili zimekuwa tofauti na za duru la kwanza, na kwa sababu hiyo kila timu inatakiwa 'kusoma ubora' wa mpinzani kwa ajili ya kufanyia kazi kabla haijakutana naye.

Vivier alisema amebaini Mbeya City wameimarika baada ya kurekebisha madhaifu yao na kazi yake ni kujipanga kukabiliana na kikosi kilichojengeka na kilicho tayari kusaka ushindi.

"Hakuna mechi rahisi, hii ni hatua ya lala salama katika ligi, benchi la ufundi na wachezaji tunatakiwa kuwa makini na kuwasoma wapinzani kiufundi na kuangalia tunaingia na mbinu gani ili kupata pointi muhimu katika michezo yetu ikiwamo huu dhidi ya Mbeya City," alisema Vivier.

Aliongeza timu yake inahitaji pointi hizo kutoka kwa Mbeya City ili kujiondoa katika nafasi ya 10 waliyopo sasa ambayo si salama.

"Tunapishana alama chache, atakayeshinda anapanda nafasi moja juu, atakayefungwa anashuka katika msimamo. Tunatakiwa kujinasua kutoka hapa tulipo, tunajua Mbeya City watakuwa nyumbani kwao hivyo hawatacheza kwa hofu, sisi pia hatutabweteka," alisema kocha huyo.

Biashara United yenye pointi 22 iko katika nafasi ya 10 wakati vinara wa ligi hiyo ni Yanga wenye pointi 51.



Kocha Mkuu wa Ngwaru FC, Mrisho Mpuna (kushoto), akitoa maelekezo kwa wachezaji wa timu hiyo inayojiandaa na mechi za Ligi Daraja la Nne zinazoendelea katika Wilaya ya Muheza jijini Tanga. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# *Mayanga kuikosa Tanzania Prisons*

**Na Shufaa Lyimo**

KIUNGO wa Polisi Tanzania, Vitalis Mayanga ataukosa mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Prisons utakaochezwa Mei Mosi, mwaka huu kutokana na hali yake kutoimarika, imefahamika.

Kocha Msaidizi wa Polisi Tanzania, George Mketo aliliambia gazeti hili afya ya mchezaji bado haijakaa sawa na hivyo benchi la ufundi limemtoa kwenye mipango yake.

"Tunasikitika tutamkosa Mayanga katika mchezo wetu dhidi ya Tanzania Prisons, kwa sababu mpaka sasa hali yake sio nzuri, hajawa tayari kukabiliana na ushindani uliopo uwanjani," alisema Mketo.

Kocha huyo alisema kikosi chake kinaendelea vyema na mazoezi kwa ajili ya mchezo huo na wameandaa programu maalumu ya kuwanoa washambuliaji ambao bado wameonekana kuhitaji kupigwa msasa.

"Safu ya ushambuliaji bado ina shida, ndio inatusababishia kutopata matokeo mazuri katika michezo iliyopita, tunatengeneza nafasi nyingi za wazi lakini tunashindwa kuzitumia vyema," Mketo alisema.

Aliongeza bado malengo yao ni kumaliza msimu huu wakiwa kwenye nafasi tatu za juu na hatimaye kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 24/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 1992 | Salernitana vs Fiorentina | 4.86 | 3.92 | 1.62 |
| 13:30 | 4774 | Keciorengucu vs Menemen Bld | 1.64 | 3.79 | 4.38 |
| 13:30 | 5560 | Boluspor vs Umraniyespor | 3.45 | 3.25 | 1.99 |
| 14:00 | 2743 | Rubin Kazan vs Arsenal Tula | 2.16 | 3.12 | 3.37 |
| 14:00 | 5237 | Rennes vs Lorient | 1.45 | 4.49 | 6.19 |
| 15:15 | 5133 | St. Gallen vs FC Lugano | 1.97 | 3.48 | 3.58 |
| 15:30 | 3912 | Groningen vs Heracles Almelo | 2.05 | 3.21 | 3.55 |
| 15:30 | 5316 | Feyenoord vs Utrecht | 1.37 | 4.99 | 6.78 |
| 16:00 | 1501 | Nice vs Troyes | 1.61 | 3.84 | 5.19 |
| 16:00 | 2212 | Brighton vs Southampton | 2.13 | 3.22 | 3.32 |
| 16:00 | 2217 | IK Brage vs Brommapojkarna | 2.40 | 3.39 | 2.88 |
| 16:00 | 2655 | Raufoss vs Grorud IL | 1.65 | 3.89 | 4.19 |
| 16:00 | 2738 | Kocaelispor vs Manisa BBSK | 2.91 | 3.16 | 2.27 |
| 16:00 | 2991 | Yeni Malatyaspor vs Konyaspor | 5.18 | 3.93 | 1.59 |
| 16:00 | 3581 | Metz vs Brest | 2.88 | 3.18 | 2.42 |
| 16:00 | 3740 | Bologna vs Udinese | 2.77 | 3.17 | 2.48 |
| 16:00 | 3844 | Burnley vs Wolverhampton | 2.72 | 2.91 | 2.72 |
| 16:00 | 3879 | Empoli vs Napoli | 4.87 | 4.07 | 1.59 |
| 16:00 | 4886 | Chelsea vs West Ham | 1.52 | 4.09 | 5.58 |
| 16:00 | 5645 | Nantes vs Bordeaux | 1.77 | 3.63 | 4.27 |
| 16:00 | 5799 | Clermont Foot vs Angers | 2.23 | 3.24 | 3.14 |
| 16:00 | 5934 | Basaksehir vs Hatayspor | 1.66 | 3.68 | 4.97 |
| 16:30 | 1457 | Rostov vs Spartak Moscow | 2.97 | 3.22 | 2.31 |
| 16:30 | 4313 | VfL Bochum vs Augsburg | 2.26 | 3.16 | 3.11 |
| 17:30 | 2433 | Grasshoppers vs Lausanne-Sport | 2.02 | 3.53 | 3.38 |
| 17:30 | 5144 | FC Basel vs FC Luzern | 1.78 | 3.79 | 3.99 |
| 17:45 | 4643 | Fortuna Sittard vs GO Ahead Eagles | 2.31 | 3.16 | 3.02 |
| 18:05 | 4747 | Lille vs Strasbourg | 2.24 | 3.23 | 3.13 |
| 18:30 | 4044 | Helsingborg vs BK Hacken | 3.06 | 3.21 | 2.17 |
| 18:30 | 4355 | Liverpool vs Everton | 1.17 | 6.70 | 12.81 |
| 18:30 | 4755 | Hertha BSC vs Stuttgart | 2.78 | 3.22 | 2.44 |
| 19:00 | 2040 | Viking vs Bodo Glimt | 2.63 | 3.47 | 2.46 |
| 19:00 | 2205 | Kristiansund vs Ham-Kam | 2.05 | 3.38 | 3.43 |
| 19:00 | 2392 | Tromso vs Sarpsborg | 2.17 | 3.23 | 3.28 |
| 19:00 | 3269 | Valerenga vs Jerv | 1.32 | 5.16 | 8.13 |
| 19:00 | 4136 | Genoa vs Cagliari | 2.17 | 3.13 | 3.33 |
| 19:00 | 5770 | Lillestrom vs Haugesund | 1.63 | 3.83 | 4.97 |
| 19:30 | 4748 | Universidad Catolica vs Colo Colo | 3.02 | 3.22 | 2.18 |
| 19:30 | 5489 | CSKA Moscow vs Dinamo Moscow | 2.36 | 3.21 | 2.91 |
| 19:30 | 5932 | Lugo vs Leganes | 2.73 | 2.88 | 2.73 |
| 20:00 | 1356 | GD Estoril vs Belenenses | 1.79 | 3.28 | 4.76 |
| 20:30 | 2188 | Altay vs Galatasaray | 3.94 | 3.50 | 1.87 |
| 20:30 | 3220 | Istanbulspor vs Erzurum BB | 2.36 | 3.22 | 2.73 |
| 20:30 | 3827 | Balikesirspor vs Ankaragucu | 15.58 | 6.04 | 1.15 |
| 20:30 | 5852 | Antalyaspor vs Kayserispor | 1.77 | 3.57 | 4.37 |
| 21:00 | 4034 | Rosenborg vs Molde | 2.41 | 3.39 | 2.74 |
| 21:15 | 4234 | Luka Koper vs Olimpija Ljubljana | 2.63 | 3.16 | 2.48 |
| 21:45 | 1122 | Reims vs Marseille | 3.69 | 3.29 | 2.00 |
| 21:45 | 5332 | Lazio vs AC Milan | 2.83 | 3.28 | 2.37 |
| 22:00 | 5333 | Barcelona vs Rayo Vallecano | 1.35 | 4.97 | 7.92 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Aprili 24, 2022

Nipashe





Ralf afunguka hatima ya Pogba UKURASA 21


# Simba SC, Orlando muda umefika

## ●●● Pablo asisitiza yuko tayari kuhakikisha anafuzu nusu fainali na...

**Na Adam Fungamwango**

NI kusuka au kunyoa kwa wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Simba watakaposhuka kwenye Uwanja wa Orlando mjini Soweto leo saa 1:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki kucheza mechi ya mkondo wa pili dhidi ya wenyeji Orlando Pirates ya Afrika Kusini.

**Simba itaingia uwanjani ikiwa na mtaji wa bao 1-0 walioupata Jumapili iliyopita katika mechi ya mkondo wa kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, kupitia penalti iliyofungwa na beki, Shomari Kapombe.**

Itakuwa na faida ya kurejea kwa wachezaji wawili, kiungo, Sadio Kanoute na beki, Joash Onyango ambao walikuwa na kadi tatu za njano, huku nahodha John Bocco kwa mujibu wa Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally akiwa amerejea kutoka kwenye majeraha.

Hata hivyo nahodha huyo ana uwezekano mdogo wa kucheza kutokana na kutokuwa sawa katika utimamu wa mwili, kwani hajacheza mechi yoyote ile hivi karibuni.

Hata hivyo itamkosa mchezaji wake tegemeo ambaye amekuwa akiibeba timu kwenye michuano ya kimataifa kwa msimu huu, Bernard Morrison kutokana na matatizo na Idara ya Uhamiaji nchini humo.

Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco alisema jana wamejiandaa vya kutosha na sasa kilichobaki ni kile walichokifanyia mazoezi kukiwasilisha uwanjani.

Pablo alisema kazi kubwa ilikuwa ni kutengeza mazingira ya kuimarisha ulinzi kwani mechi ya leo ni ngumu zaidi kuliko ile ya kwanza.

"Lazima tubadilike, tunatakiwa kucheza kwa kasi dakika 15 za mwanzo ili kupata bao la mapema ambalo litawachanganya, lakini pia kuimarisha ulinzi, ingawa najua mechi itakuwa ngumu, nimewaandaa vijana wangu," alisema Pablo.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema ana matumaini ya kufanya vyema katika mchezo huo muhimu katika kufikia malengo.

"Tumefika, tunajiandaa, tuko vitani na tunashinda," alisema Barbara.

Simba itajaribu kutaka kuweka rekodi yake yenyewe iliyoweka mwaka 1993 ilipofanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, ikiwa ugenini nchini Algeria ilipocheza dhidi ya USM El Harrach licha ya kuchapwa mabao 2-0, lakini ikiwa na mtaji wa mabao 3-0 iliyoyapata nchini kwenye mechi ya mkondo wa kwanza, hivyo kutinga hatua hiyo kwa jumla ya mabao 3-2.

Ni mwaka ambao Simba ilitinga hatua ya fainali na kufungwa mabao 2-0 dhidi ya Stella Abidjan kwenye mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru), huku mechi ya kwanza ikiwa ugenini ikilazimisha suluhu.

Wawakilishi hao wa Tanzania itakuwa ni mara ya pili kucheza Afrika Kusini, mwaka 2003 kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, ilikipiga dhidi ya Santos FC ya nchini humo kwenye Uwanja Athlone, Aprili 13, mwaka 2003 na ikalazimisha suluhu na mechi ya marudiano nchini ikichezwa Aprili 27, timu hizo zilitoka tena sare na Simba kusonga mbele ya michuano hiyo kwa penalti 9-8.

Ni mwaka ambao ilitinga kwa mara ya kwanza hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya mechi iliyofuata kuwavua ubingwa wa Afrika, Zamalek na kusonga mbele.

Timu hizi zimeingia kwenye hatua ya robo fainali baada ya kutoka kwenye makundi mawili tofauti, Simba ikitoka Kundi D kwa kushika nafasi ya pili baada ya kujikusanyia kwa pointi 10 wakati Orlando Pirates iliyokuwa kwenye Kundi B, ilimaliza hatua hiyo ikiwa na pointi 13.



Beki wa Simba, Henock Inonga akijaribu kumiliki mpira katika mazoezi ya kujiandaa kuivaa Orlando Pirates katika mechi ya marudiano ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Orlando mjini Soweto, Afrika Kusini. **PICHA: SIMBA SC**

# Nabi 'out'

**Na Saada Akida**

WAKATI uongozi wa Yanga ukisema unahitaji kupata siku sita ili kukamilisha maandalizi ya kumkabili mtani wao, Kocha wake Mkuu, Nasreddine Nabi ataikosa Simba.

Yanga inatarajia kuikaribisha Simba katika mechi ya mzunguko wa pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Aprili 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Nabi ambaye alitolewa nje kwa kadi nyekundu katika mechi ya Kombe la FA dhidi ya Geita Gold FC, amebainika ametenda makosa ya kinidhamu na hivyo amefungiwa michezo mitatu na kutozwa faini ya Sh. 500,000.

Kocha huyo wa Yanga amekuwa na hatia baada ya kuwashambulia waamuzi kwa lugha ya matusi wakati wakiwa wanatimiza majukumu yao.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze alisema siku sita zinatosha kuwapatia wachezaji wao mbinu za mwisho za ushindi na wanaamini watafuata maelekezo watakayowapatia ili kuondoka na pointi tatu muhimu.

"Malengo yetu msimu huu ni kutwaa ubingwa, kuhusu muda na maandalizi ya mechi ya Simba, siku sita zinatosha kwa ajili ya kumaliza programu zetu kwa sababu kila mechi kwetu ni fainali na maandalizi ya mechi hii ni tofauti na nyingine," alisema Kaze.

Aliongeza mechi za Ligi Kuu zimeendelea kuwa na ushindani mkubwa kwa sababu kila timu imejiimarisha kuvuna pointi na kufikia malengo yake.

"Mechi hiyo ni muhimu, tutahakikisha tunafanikiwa kupata pointi tatu, tunajua Simba wako vizuri kila idara, sisi pia tunahitaji kutumia vizuri siku sita za maandalizi kwa ajili ya kujiimarisha kila idara," Kaze aliongeza.

Alisema kila mchezaji wa Yanga anafahamu umuhimu wa kupata ushindi katika mchezo huo ambao utasaidia kuwaimarisha kwenye mbio zao za kuivua Simba ubingwa.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >